Nipashe
Alhamisi Oktoba 19, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581468
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US






# Hofu yatanda nauli kupanda

• **Mapendekezo** yatua LATRA, Chalamila, wadau wasema...

*Endelea ukurasa 2*

**Adaiwa** kuua mumewe kwa mundu

UKURASA 4

**TPA** yafungua ofisi makasha Zimbabwe

UKURASA 5

**Hamas**, Israel watupiana mpira shambulio la hospitali

UKURASA 19



# Rais Samia ashtushwa bei kubwa za vyakula

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akiulizia bei ya samaki wa kukaanga katika Soko la Wamachinga Parking, Nzega Mjini, mkoani Tabora jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 4

## JAFO AZINDUA MWONGOZO TATHMINI MAZINGIRA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira...

## Mwekezaji akabidhiwa Bandari ya Malindi

UKURASA 3

MICHEZO **SAMIA ANOGESHA MECHI YA SIMBA AFL** UK.24 **KABWELA** UK.7

# Hofu yatanda nauli kupanda

**Na Waandishi Wetu**

HOFU ya kupanda nauli imetanda miongoni mwa wananchi baada ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kukutana na wadau wa usafirishaji kujadili mapendekezo ya viwango vya nauli mpya.

Jana, wadau wa usafirishaji waliwasilisha mapendekezo yao kwa LATRA ya kuomba kupandisha nauli, huku wakisisitiza kwamba kupanda kwa nauli hizo hakuepukiki.

Miongoni mwa sababu kubwa za wadau hao kuomba kupanda kwa nauli hizo ni kuadimika na kupanda kwa dola ambayo wanaitumia katika shughuli za uendeshaji zikiwamo kupanda kwa mafuta na vifaa vyote vya magari ambavyo vingi wanaviagiza nje ya nchi.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), Priscus Joseph, alisema katika kipindi cha miezi mitatu pekee, mafuta yamepanda kwa ongezeko la Sh.1,000.

"Mafuta yanapanda kila mwezi lakini mchakato wa kupandisha nauli unachukua muda mrefu. Tunaomba hata sheria ibadilike na iwe na kipindi cha dharura cha kupandisha nauli inapotokea hali kama hii ya sasa. Juni, mwaka huu, mafuta yalikuwa Sh.2,500 lakini sasa ni Sh.3,500, ongezeko la Sh. 1,000," alisema.

Joseph alisema kilio chao ni kuomba wawekewe ruzuku ili isaidie kupunguza makali hayo ya gharama za mafuta na kupanda kwa maisha ya wananchi na kushauri kufanyike maboresho ya sheria mbayo itaweka vipengele vya kupandisha nauli kunapotokea nyakati za dharura kama sasa.

Katibu Mkuu huyo pia alishauri kuongeza vituo nchi nzima vya usambazaji gesi asilia ili kusaidia kupunguza uhitaji wa mafuta.

Mwenyekiti wa Wamiliki wa Daladala Mkoa wa Dar es Salaam (DARCOBOA), Sabri Mabrouk, alisema mapendekezo yao kwa nauli za daladala wameomba kupanda kutoka Sh. 500 hadi Sh.800 kwa umbali wa kilomita 20, wameomba ipande hadi Sh. 1,600, kilomita 30 Sh. 2,400 na kilomita 15 kwa Sh. 1,200.

### KAULI YA CHALAMILA

Kutokana na mapendekezo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, aliishauri LATRA kuyafanyia kazi itakavyoona inafaa pasipo kumiza upande mmoja.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alisema wamepokea mapendekezo hayo na watayafanyia kazi ikiwamo kuyapeleka kwenye bodi ambayo nayo itayafanyia tathmini ya kuyapeleka wizarani kwa hatua zaidi.

### HOFU YATANDA

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba (JUKATA), Dk. Ananilea Nkya, alisema endapo nauli itapanda, gharama za maisha zitapanda maradufu na kuongeza mzigo kwa mwananchi.

Akizungumza na Nipashe jana, alisema hali hiyo itasababisha baadhi ya huduma kama vyakula kupanda, hivyo kusababisha matatizo ya chakula kwa baadhi kushindwa kuhimili milo mitatu kwa siku.

"Tutarajie ongezeko la watu wenye msongo wa mawazo kwa sababu maisha yamepanda, ajira hakuna," alisema.

Musa Hamduni, dereva wa daladala kati ya Ubungo na Gongo la Mboto, alisema biashara inakuwa ngumu siku hadi siku kutokana na mafuta kuwa juu.

"Gari aina ya Toyota Coaster ruti ndefu, zamani hesabu hata ukiambiwa Sh. 120,000 una uhakika wa kuipata lakini sasa wanalia. Bora hata sisi wenye (Toyota) DCM kidogo hazili mafuta. Madereva wa Coaster hata hesabu ya Sh. 100,000 kwa siku mtihani, bado faini za barabarani," alisema.

Mmiliki wa gari ndogo ya binafsi, Abdallah Mwano, alisema hivi sasa inamlazimu kutumia Sh.30,000 kwa siku safari ya kwenda kazini na kurudi nyumbani huku akibainisha kuwa awali alikuwa akitumia wastani wa Sh. 15,000.

Mwenyekiti wa Chama cha Kutetea Abiria (CHAKUA), Hassan Mchanjama, alisema endapo nauli zitaongezwa, kutakuwa na madhara ya moja kwa moja kwa wananchi ambao ni abiria.

Alisema Watanzania wengi kipato chao ni cha chini, hivyo kuongezeka kwa nauli kutasababisha wengine kushindwa kumudu uendeshaji wa shughuli zao, hasa wale ambao wanalazimika kufanya safari za mara kwa mara kwenda kwenye majukumu yao.

"Kuna haja kwa serikali kusaidia wananchi kwa sababu ndio wanaoumia pindi nauli zinapoongezeka, vinginevyo wananchi wataendelea kutupia lawama serikali juu ya kuongezeka kwa gharama za usafiri," alisema.

Mhadhiri na Mtaalamu wa Biashara na Uchumi kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Mariam Tambwe, alisema suala hilo litasababisha madhara kiuchumi kwa sababu ongezeko la nauli pia litakuwa mzigo kwa wananchi pamoja na kupanda kwa bei ya bidhaa.

"Nauli zitaongezeka lakini mishahara iko pale pale, hivyo serikali iangalie pande zote mbili kwa sababu mafuta yakiwa juu wasafirishaji watashindwa kuendesha biashara zao. Pia wananchi watashindwa kufanya shughuli zao," alisema.

Mwanaharakati wa masuala ya kisiasa na kijamii, Bubelwa Kaiza, alisema endapo LATRA itapandisha nauli itakuwa sahihi kwa sababu bei ya mafuta inapanda kila mwezi.

"Ni vitu vingi vimepanda na wenye magari nao wanatakiwa kurudisha faida. Shida ipo hapo kama wanataka kupandisha nadhani wako sahihi," alisema na kuongeza kuwa uchumi hauathiriwi kutokana na kupanda kwa bei peke yake bali kwa mambo mengi.

"Kimsingi mpaka sasa wananchi wameshaathirika. Ukienda madukani bidhaa mbalimbali zimepanda bei. Chakula kimepanda, mazao yamepanda kutokana na bei za mafuta kupanda kila mwezi," alisema.

Kaiza alisema kitu ambacho serikali inatakiwa kufanya ili kuondoa athari hizo ni kuweka sera na sheria kusaidia, badala ya magari mengi kutegemea mafuta yatumie gesi.

***• Imeandaliwa na Elizabeth Zaya, Christina Mwakangale, Maulid Mbaga na Beatrice Shayo***



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, ACP Theopista Mallya, akiteta na mtoto wa Shule ya Msingi Haloli, baada ya kutoa elimu kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa watoto shuleni hapo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Utafiti wabaini tatizo afya akili kwa wagonjwa wa moyo

**Na Christina Mwakangale**

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), kwa wagonjwa watano ambao wamewekewa betri (pace maker) kwenye moyo, umebaini wanapitia changamoto za afya ya akili.

Hali hiyo imeelezwa inatokana na watu hao kutojiandaa kifikra katika kuipokea tiba hiyo.

Matibabu ya kuwekewa betri kwenye moyo huidhinishwa na madaktari bingwa, baada ya uchunguzi kufanyika kwa mgonjwa ili kusaidia kurekebisha mfumo wa umeme na kuokoa maisha.

Daktari Bingwa wa Moyo na Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Mafunzo JKCI, Dk. Pedro Pallangyo, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu matokeo ya utafiti yaliyotolewa na taasisi hiyo iliyoitwa: Changamoto ya Afya ya Akili kwa Wagonjwa Waliowekewa Betri Kwenye Moyo'.

Dk. Pallangyo alisema wagonjwa hao walikutwa na dalili za magonjwa tofauti ya akili na kisha kuhatarisha mfumo wa matibabu ya moyo kutokana na kutotengemaa kwa afya ya akili.

"Utafiti tofauti duniani umeonyesha kwamba wagonjwa wanaowekewa vifaa (betri) wanapopata matatizo ya akili na wakagundulika au kutibiwa mapema, wana uwezekano mkubwa wa kutozingatia ushauri wa kiafya waliopewa, kama vile kubadili mfumo wa maisha na uzingatiajia wa dawa.

"Utafiti huu unalenga kuiasa jamii na watoa huduma, madaktari, wauguzi, kuwa makini na kuhakikisha wagonjwa wote kabla ya kuwekewa hivi vifaa au kufanyiwa upasuaji, wanafuatilia mfumo wao wa akili au afya ya akili, ili waweze kuingilia kati kwa maana ya matibabu, kwa sababu wagonjwa hawa wasipogundulika mapema wanaweza kupoteza maisha," alisema Dk. Pallangyo.

Alisema kwamba taasisi hiyo iliwahi kukutana na kesi ya aina hiyo, baada ya mmoja wa wagonjwa wa moyo aliyewekewa betri kwenye moyo, alijirusha ghorofani akiwa JKCI na kufariki dunia.

"Yote hii ilitokana na yeye kutojikubali au mfumo wake wa akili kutokubali na kuathiri afya yake ya akili baada ya kuwekewa betri. Wagonjwa hao huanzishiwa matibabu kutoka kwa madaktari bingwa wa magonjwa na afya ya akili."

HABARI KITAIFA

# AGL yakabidhiwa uendeshaji Bandari ya Malindi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Muhammed, amesema Serikali ya Zanzibar imeona ipo haja ya kuingia mkataba na kampuni yenye uzoefu, uwezo na utaalamu wa kuendesha na kusimamia Bandari ya Malindi ili kuleta ufanisi.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya uendeshaji wa bandari hiyo kwa kampuni ya Africa Global Logistics (AGL), alisema baada ya taratibu zote za mchakato wa zabuni kukamilika, kampuni ya AGL ya Ufaransa ilishinda zabuni ya uendeshaji na usimamizi wa bandari hiyo na serikali kuingia mkataba na kampuni hiyo Mei 23, mwaka huu.

Alisema baada ya masharti yote kukamilika, Shirika la Bandari Zanzibar lilikabidhi jukumu la uendeshaji na usimamizi wa bandari hiyo kwa kampuni ya AGL Septemba 23, mwaka huu.

"Leo ni makabidhiano rasmi, lakini mkataba huu wa miaka mitato una maeneo makuu matano, moja ni kuboresha miundombinu na huduma katika bandari hii, pili kujenga bandari kavu katika eneo la Maruhubi, tatu kuwajengea uwezo watendaji wetu 400 wa Shirika la Bandari, nne kuongeza ufanisi wa utoaji huduma na kuwekeza katika vifaa, mafunzo na mifumo na tano ni kuhakikisha tunatimiza matakwa ya kimataifa katika kuweka mazingira salama ya utoaji huduma kwa wateja," alisema.




Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Muhammed (wa pili kulia), akikabidhi rasmi shughuli za uendeshaji wa Bandari ya Malindi kwa Rais wa Kampuni ya AGL, Philippe Labonnt, katika hafla iliyofanyika bandarini hapo, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Aidha, alisema ukodishwaji huo utaongeza ufanisi wa shughuli za uendeshaji wa bandari hiyo na serikali chini ya uongozi wa Rais Dk. Mwinyi amefanya jitihada kubwa ya kutafuta mbinu ya kutatua changamoto zilizokuwapo katika bandari hiyo ambayo ndiyo lango kuu la kiuchumi.

Alisema lengo na azma ya Rais Dk. Mwinyi kuitoa bandari hiyo ni kwa ajili ya kuongeza ufanisi, hasa ikizingatiwa kuwa bandari hiyo ni ya muda mrefu toka mwaka 1960 ilipojengwa na bado ndiyo lango kuu la kiuchumi Zanzibar.

"Mahitaji yameongezeka, biashara imekua, mizigo inayokuja Zanzibar na kwenda sehemu nyingine imeongezeka, tulikuwa tunakabiliwa na ufinyu wa nafasi katika bandari hii, tumekuwa na msongamano mkubwa wa makontena, lakini meli zikikaa muda mrefu kwa muda wa siku 42 meli imekaa katika ukuta inasubiri kushusha mzigo," alisema.

Alisema changamoto hizo ni kiashiria cha ufanisi mdogo katika shughuli za uendeshaji wa bandari ambao unasababisha kuongezeka kwa gharama za kuingiza mzigo, kuleta hasara kubwa kwa uchumi wa nchi na kupanda kwa gharama za bidhaa.

Alisema bei za kusafirisha na kushusha mizigo Zanzibar zilikuwa juu ikilinganishwa na bandari zingine za Tanzania bara na Mombasa-Kenya na wakati mwingine ilisababisha meli kukataa kufika Zanzibar kwa kuhofia kukaa muda mrefu na ni gharama kubwa.

Dk. Khalid alisema katika kukabiliana na changamoto hizo serikali imeandaa mipango yenye lengo la kuongeza ufanisi na kuifanya Zanzibar kuwa kituo kikuu cha usafirishaji wa mizigo kwa nchi jirani na kukuza uchumi wa nchi.

Alisema miongoni mwa mipango hiyo ya muda mfupi ni kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa Bandari ya Malindi kwa kuongeza vifaa, uwekaji wa mifumo ya TEHAMA na kuwa na usimamizi madhubuti wa shughuli zote za bandari.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya ZMT, Nicolas Escalin, aliwataka wafanyakazi watakaofanya kazi na kampuni hiyo kuwajibika kikamilifu kwa ajili ya kuona matarajio ya serikali na kampuni yanafikiwa.

Aliyataja baadhi ya mambo wanayotarajia kuyafanya ni kuwajengea uwezo wafanyakazi, kufanya kazi katika mazingira ya sayansi na teknolojia na kampuni hiyo itazingatia usawa wa kijinsia katika utendaji wa kazi zao.

"Katika kipindi cha miezi minne tunatarajia kujenga bandari kavu hapo Maruhubi ambayo itapunguza msongamano wa mizigo katika bandari ya Malindi," alisema.

Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, alisema Zanzibar inaelekea pazuri katika mikakati yake ya kuimarisha uchumi na biashara kwa kampuni kubwa duniani.

Alisema mazingira ya uwekezaji Zanzibar ni mazuri na yanatoa fursa kwa kampuni binafsi kufika Zanzibar kuwekeza na kutoa mchango wao kiuchumi.

# Samia ashtushwa gharama bei za vyakula

**Na Vitus Audax,** NZEGA

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alitembelea Soko la Nzega Parking, mkoani Tabora na kushtushwa na gharama ya bei ya vyakula hasa samaki na nafaka.

Rais Samia ambaye anaendelea na ziara yake mkoani humo, alifanya ukaguzi wa mradi mkubwa wa skimu ya umwagiliaji wa mbegu Kilimi 'Mama Samia Skimu' uliotekelezwa wilayani Nzega kwa zaidi ya Sh. bilioni 6.2.

Baada ya ukaguzi na kuweka jiwe la msingi katika mradi huo, Rais Samia alitembelea soko hilo na kutaka kujua hali ya biashara sokoni hapo na bei ya bidhaa na kuambiwa kuwa kwa mamalishe chakula kinauzwa sahani moja ya wali na maharage kuanzia Sh. 1,500 hadi 2,000.

Aidha, alishtushwa na bei ya samaki wadogo aina ya sangara waliokuwa wakiuzwa na wafanyabiashara wadogo, mmoja kwa Sh. 1,000 na alipopiga hesabu alibaini kuwa kwa familia ya watu watano ilihitaji kuwa na Sh. 5,000 kwa ajili ya samaki pekee.

"Huyu samaki elfu moja, watoto watakula kweli, inamaanisha watoto wangu watano ni Sh. 5,000 kwa samaki tu, sina unga wa ugali, sina viungo vya mboga sasa mimi nitakula kweli leo?" Alihoji.

Wafanyabiashara hao walisema wanauza bei hiyo kwa sababu hata wao wanakowachukua huuziwa kwa bei ghali kutoka soko la samaki mkoani hapo maarufu 'Kariakoo' ambao hununua hadi Sh. 2,000 na zaidi.

Kadhalika vitunguu viliuzwa kwa Sh. 10,000 kwa kisado kimoja huku kilo moja ikiuzwa kwa Sh. 3,000, karanga kilo moja Sh. 2,500, mchele ulianzia Sh. 2,500 kwenda juu huku bei ya nyanya fungu moja likiuzwa kwa Sh. 500.

Pia wafanyabiashara hao, walimwambia Rais Samia kuwa hali zao kibiashara ni mbaya kutokana na kila siku vitu kupanda bei na wateja kukosekana.

"Biashara kwa sasa imekuwa ni ngumu, upatikanaji wa fedha ni mgumu ni sawa watu wamevuna, lakini fedha ilipoenda hatufahamu, bidhaa zipo juu, hata hivyo wateja kuwapata ni ngumu," alilalamika mmoja wa wafanyabiashara hao.

Vile vile, katika soko hilo, Rais Samia alibaini ubovu na uchakavu wa miundombinu na kumwagiza mbunge wa jimbo hilo ambaye pia ni Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe kuhakikisha ukarabati unafanyika.

"Kwa kuanzia serikali imetenga Shilingi bilioni nne kwa ajili ya ukarabati wa soko hili, hivyo mbunge na mkuu wa wilaya mtatueleza mikakati juu ya zoezi hili na soko litakapokamilika wa kwanza kuwarudisha hapa wawe ni wale mliowakuta sio kuleta matajiri tu hapa," alionya.

Katika ziara hiyo, Dk. Samia alitoa mitaji kwa wafanyabiashara mbalimbali ambao walieleza biashara zao kudorora kutokana na ufinyu wa mitaji na kuagiza zaidi ya Sh. milioni 1.5 itolewe kwa wafanyabiashara hao ili kuwasaidia kuinua mitaji na shughuli zao.

Rais Samia pia aliongea na wananchi katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na eneo la Puge Nzega Vijijini na Magili lililopo Tabora Kaskazini.

Mbunge wa Nzega Vijijini, Hamis Kigwangala, alimwomba Rais Samia wakati akiendelea kufikiria Nzega kuipa hadhi ya mkoa, basi awasaidie wananchi wake kupata halmashauri mbili ya Bukene na Nzega ili kuondoa adha ya kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma za kiserikali.

Mbunge wa Tabora Kaskazini, Athumani Maige, aliishukuru serikali kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuidhinisha Sh. bilioni 47.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo huku akiwasilisha ombi la ujenzi wa barabara ya lami ya Magili-Kigwa yenye urefu wa kilomita 27 kusaidia kuunganisha wananchi na halmashauri.

Katika maombi hayo Rais Samia alisema yatafanyiwa kazi katika bajeti ya 2024/25 kwa kuwa kwa sasa tayari bajeti imepangwa na inaendelea kutekeleza miradi mingine.

Alisema, wanatambua uhitaji wa wananchi hao na kuahidi kuifanyia kazi mapema iwezekanavyo.


FOR IMMEDIATE RELEASE

**Queen Geofrey, CEO, takes over Backlite, Dar es Salaam – a surprise move within Dar es Salaams media world!**

Queen Geofrey, the CEO of BackLite Media takes over a principal stake in the high quality outdoor advertising company and changes the name to Starlite Vision Limited.

Starlite will continue the company's successful installation and marketing of exclusive backlit signs in the capital.

- " I am delighted to take over and continue the business with high quality advertising signs at the JNIA International Airport and in the city centre of Dar es Salaam, Queen Geofrey said yesterday, when the news was published."
- " I have been 15 years within this field of business and I have seen the growing demand of quality signs from clients."

Queen Geofrey was before the General Manager in BackLite and she is now the CEO of Starlite Vision:

- " We plan to build another 4 signs at the International Terminal III, where we now can see a growing demand after the hard pandemic years.
- In the city centre we have two Double Decker signs at Bagamoyo Road and the region's largest high quality digital sign at Uhuru Park, The Prime Digital.
- We will also start the installation of another Double Decker sign at foot of the Tanzanite Bridge.

**For further information contact Queen Geofrey on +255 687 206 226 or via email address queen@starlitevision.tz**

# Adaiwa kumuua mume kwa mundu akimzuia kumwadhibu mtoto wao

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi mkoani Njombe, linamshikilia Tressfolina Nkolongo (33), mkazi wa eneo la Viziwi Kata ya Mji Mwema, Halmashauri ya Mji wa Njombe, kwa madai ya kumuua mume wake, Bosco Mhagama (53) kwa kumpiga na mundu kichwani ili kumzuia asimwadhibu mtoto.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Octoba 16, mwaka huu, majira ya saa 5:00 usiku na kwamba mtuhumiwa alifanya hivyo katika kumzuia mume wake kumwadhibu mtoto.

"Chanzo chake ni mwanamke huyu kumpiga mumewe na nyengo (mundu) kichwani wakati akimzuia mumewe kuendelea kumpiga mtoto," alisema.

Kamanda Banga alisema mtuhumiwa atafikishwa mahakamani wakati wowote baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Julius Kiswaga mkazi wa Mji Mwema ambaye ni jirani wa familia hiyo, alisema Mhagama alikuwa na tabia ya kumpiga mke wake mara kwa mara.

"Tujitahidi kushusha hasira ya ghafla kwa sababu kama sasa hivi familia inabaki peke yake mama yuko gerezani na baba kaburini," alisema Kiswaga.

Diwani wa Mji Mwema, Nestory Mahenge, aliwasihi wananchi wa kata hiyo kujitahidi kuishi kwa upendo na mshikamano pamoja na kuwa na hofu ya Mungu.

"Kwenye kata yangu pia kumekuwa na kukithiri vitendo vya ukatili na unyanyasaji. Kwa ujumla nawasihi watu wasijichukulie sheria mkononi pale ambapo kuna changamoto na migongano kwani kuna ngazi za usuluhishi," alisema Mahenge.



Mfanyabiashara wa matikiti maji, Fred Burasha (kushoto), akimhudumia mteja wake katika Soko la Vetanari Temeke, Dar es Salaam jana. Tikiti moja liliuzwa kwa 2,000/- hadi 5,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jafo azindua mwongozo tathmini mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amezindua mwongozo wa tathmini za athari kwa mazingira kwenye miradi ya majengo na kuagiza miongozo mingine iandaliwe ya sekta ya viwanda, nishati, kilimo na maji.

Jafo alisema hayo jijini hapa alipokuwa akizindua mwongozo huo ulioandaliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Kituo cha Sayansi na Mazingira cha India (CSE).

Alisema mwongozo huo umezingatia mahitaji halisi ya nchi ikiwamo ukuaji wa miji na majiji, limeipa NEMC mamlaka ya kuhakikisha hali ya mazingira inaboreshwa kwa kusaidia uboreshaji wa afya ya jamii ikiwa ni pamoja na mazingira vinalindwa na kuweka mazingira bora ya uwekezaji nchini.

Waziri Jafo alisema kipengele namba 17 cha makubaliano ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu maendeleo endelevu unazitaka nchi wanachama kuhusisha tathmini za athari za mazingira katika miradi ambayo inasababisha madhara kimazingira.

"Tathmini za athari kwa mazingira (TAM) hufanyika ili kuweka mifumo bora ya kulinda mazingira ikiwa ni pamoja na kupunguza kiwango cha taka zinazozalishwa, kutoa kipaumbele katika masuala ya jamii, kuainisha athari zilizopo na madhara yanayoweza jitokeza kutokana na miradi inayoanzishwa," alisema.

Alibainisha kuwa NEMC inapokea zaidi ya miradi 2000 kwa mwaka kwa ajili ya mapitio na kuongeza kuwa idadi hiyo ya miradi ni kubwa na itaweza kupitiwa kwa ufanisi iwapo kutakuwa na miongozo ya kila sekta kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

"Niishukuru serikali ya India kupitia kituo hicho kwa kushirikiana na NEMC katika kuandaa mwongozo huu kwani ushirikiano huu ni ishara ya matokeo ya ushirikiano wa taasisi hizo katika kupatia ufumbuzi wa changamoto za kimazingira," alisema.

Naye Mkurugenzi wa India (CSE), Nivit Yadav, alisema Tanzania ni nchi ya tatu barani Afrika yenye kasi kubwa ya idadi ya watu na nchi ya pili kwa Mataifa ya Afrika Mashariki kuwa na kasi ya ukuaji wa sekta ya ujenzi, hivyo suala la tathmini ya miradi ya ujenzi ni jambo muhimu linalopaswa kupewa kipaumbele katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samwel Gwamaka, alisema kwa muda mrefu kumekuwapo na tatizo la usimamizi wa tathmini ya athari kwa mazingira kupitia maandiko ya miradi mbalimbali yanayowasilishwa kwa ajili ya utoaji wa vibali vya mazingira kutokana na kukosekana mwongozo.

## Taka majumbani fursa kwa uchumi

**Na Jenifer Gilla**

JIJI la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Taasisi ya Mazingira Plus na TACSS limezindua Mradi Shirikishi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (ICA) unaolenga kugeuza taka zinazozalishwa majumbani kuwa fursa kiuchumi.

Kupitia mradi huo, wakusanya taka zitokanazo na chakula na plastiki watapewa elimu ya kuziongezea thamani na kuzitumia katika shughuli zingine kama vile kulisha mifugo na kutengeneza urembo, hivyo kuwasaidia kujiinua kiuchumi.

Akizungumza katika uzinduzi wa mradi huo jana, Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto, alisema lengo la mradi huo ni kuzuia taka kwenda dampo ili kupunguza mrundikano wa taka katika maeneo hayo.

Kumbilamoto alisema asilimia 60 ya taka zinazozalishwa majumbani ni zile ambazo zinaoza na zinaweza kutumika katika shughuli zingine, hivyo wameona ni vyema kuwapatia elimu vikundi vya wazoa taka katika ngazi za mitaa ili watumie fursa hiyo kujiinua kiuchumi.

Alisema wamechagua kufanya kazi kwa ukaribu na wazoa taka na waokota chupa za plastiki mitaani kwa kutambua mchango wao mkubwa wanaofanya wa kuliweka jiji katika hali ya usafi.

"Dar es Salaam inatambua umuhimu wa kufanya kazi na kuwezesha jumuiya zisizo rasmi na wafanyakazi wasio rasmi ili kuunda pamoja sera na mipango endelevu ya usimamizi wa taka," alisema.

Aliishukuru Jumuiya ya Majiji Duniani (C40s ) kwa kufadhili mradi huo kupitia mfuko wa ICA ili kufanikisha utekelezaji wa mradi huo ambao pia utaimarisha ushirikiano na wazoa taka wasio rasmi na kufikia malengo waliojiwekea.

Ofisa Mazingira Mkuu wa Jiji, Monica Mosha, alisema mradi huo utatekelezwa kwa mwaka mmoja utaanzia katika Kata ya Vingunguti kisha maeneo mengine kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mosha ambaye ni mratibu wa mradi huo, alisema wameanza na kata hiyo kwa sababu ina makazi yasiyo rasmi ambayo miundombinu yake haifikiwi kirahisi na makandarasi wakubwa, hivyo kusababisha taka kutozolewa kwa wakati.

"Tunatarajia pia kutunza mazingira ambapo yakiwa masafi faida ni nyingi kama vile jiji kupendeza, hewa safi na kuwaepusha wananchi na magonjwa yatokanayo na mrundikano wa taka kikiwamo kipindupindu," alisema Mosha.

Mmoja wa wazoa taka ngumu katika kata hiyo, Elizabeth Ndunguru, alisema mradi huo utawapa fursa ya kupata elimu juu ya kubadilisha taka kuwa fursa ya kiuchumi jambo ambalo hakulifahamu mwanzoni.

Alisema pia ni matarajio yake kupitia mradi huo watapata vifaa vya kisasa vitakavyorahisisha utendaji wa kazi zao na kuwaepusha na maradhi wanayokumbana nayo mara kwa mara kutokana na kutumia vifaa visivyo na ubora unaotakiwa.

# Ilala kinara maambukizi malaria Dar

Na Maulid Mmbaga

WILAYA ya Ilala imeelezwa kuwa kinara wa ugonjwa wa malaria katika Mkoa wa Dar es Salaam ikiwa inaongoza kwa maambukizi kwa asilimia 1.7 huku Kigamboni ikiwa ya mwisho kwa kuwa na asilimia 0.5.

Mratibu wa Malaria Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Ford Chisongela, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa mpango wa kusambaza zaidi ya vyandarua 700,000 katika shule za msingi 878 za mkoa huo. Mpango huo unatekelezwa na Ofisi ya Urtatibu wa Malaria Mkoa wa Dar es Salaam kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Bohari ya Dawa (MSD).

Dk. Chisongela alisema wajawazito ambao walipima malaria mwaka 2018, wengi walikutwa na maambukizi ya ugonjwa huo lakini kutokana na jitihada zilizofanyika katika kudhibiti tatizo hilo, kwa mwaka jana hali ilishuka hadi kufikia asilimia 0.5.

Kwa wagonjwa wa nje, alisema idadi imeshuka kutoka 300,000 mwaka 2018 hadi 150,000 mwaka 2022 na wagonjwa wanaolazwa kutokana na malaria, wamepungua kutoka 154 hadi 46 huku vifo vikishuka kutoka 75 mpaka 44. Dk. Chisongela alisema Temeke ndiyo inayoongoza kwa vifo.

"Kwa upande wa mazalia ya mbu, Ilala ina mazalia 9,852, Temeke 3,511, Kinondoni 3,366, Ubungo 1,268, na Kigamboni 1,113 na afua ambazo zimefanikisha mafanikio haya ni ugawaji wa vyandarua, matibabu, udhibiti wa wadudu wadhurifu kwa kupuliza dawa kwenye mazalia.

"Mkoa wa Dar es Salaam umekuwa ukitekeleza afua hii kwa miaka 23 ikiwamo kutoa elimu ya afya namna ya kujikinga na malaria pamoja na ufuatiliaji ikiwamo utambuzi wa mlipuko wa ugonjwa," alisema.

Dk. Chisongela aliongeza kwamba katika jitihada hizo bado kuna changamoto zinazowakabili ikiwamo kiwango kikubwa cha malaria ikiwamo Kigogo Luhanga na Tundwi Songani. Alisema kwenye maeneo hayo kati ya watu 100 wanaopimwa malaria takribani watu 30 huthibitika kuwa na ugonjwa huo.

Changamoto nyingine, alisema ni bajeti ndogo ya afua ya unyunyuzaji wa viuadudu hasa kwa wilaya za Kigamboni na Ubungo.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Afya, Mercy Mpatwa, alisema katika jitihada za kudhibiti ugonjwa huo, mwaka 2022 waligawa vyandarua 800,000 katika shule za msingi mkoani Dar es Salaam na kwamba mambo waliyoyabaini kama changamoto ni ucheleweshwaji mkubwa wa fedha kwenda kwa watekelezaji katika halmashauri.

"Pia uingizwaji wa hizo taarifa ulikuwa unachelewa baada ya kuwa zimepokewa mifumo ambayo ilibidi wapate mrejesho wa kwamba nini kimefanyika. Katika mwaka huu, tumejipanga kuongeza ufuatiliaji wa karibu ili kuanzia ngazi ya halmashauri kuingiza hizo data kwa wakati," alisema Mpatwa.

Mwakilishi wa Meneja wa MSD Kanda ya Dar es Salaam, Frank Mpembeni, alisema idadi ya shule na vyandarua vitakavyosambazwa kwa mgawanyiko wa wilaya ni Ubungo shule 194 vyandarua 122,116. Wilaya zingine ni Kigamboni shule 77 ambayo itapatiwa vyandarua 44,311, Temeke 152 (vyandarua 180, 843), Kinondoni 175 (vyandarua 106,123) na Ilala 280 itakayo gawiwa vyandarua 255,725.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alishauri kuwapo utamaduni wa kudhibiti mbu wakiwa wadogo kabla ya kufikia katika hali ya ukomavu. Pia alisema serikali imeleta wawekezaji wakiwamo kutoka Cuba wanaotengeneza dawa za viuadudu ambazo wanaweza kuzitumia kupuliza mji wote ili uwe salama.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (wa tatu kushoto), akipokea mfano wa vyandarua kutoka kwa Mwakilishi wa Meneja wa Bohari ya Dawa (MSD) Ukanda huo, Frank Mpembeni (kulia), wakati wa uzinduzi wa mpango wa kusambaza vyandarua 709,118 katika shule za msingi 878 za mkoa huo jana, ikiwa ni mwendelezo wa jitihada za kupambana na ugonjwa huo. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# TPA yafungua ofisi Zimbabwe kurahisisha usafirishaji shehena

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imezidi kuboresha huduma zake barani Afrika kwa kufungua ofisi nyingine nchini Zimbabwe na kurahisisha usafirishaji shehena za mizigo moja kwa moja kutoka Bandari ya Dar es Salaam kupitia Bahari ya Hindi.

Hatua hiyo imekuja baada ya TPA kufungua ofisi zake katika nchi jirani na Tanzania za Rwanda, Burundi, Uganda, Zambia, Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Akizungumza wakati wa hafla ya kufungua ofisi hiyo mjini Harare mwanzoni mwa wiki hii, Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa alisema pamoja na kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na Zimbabwe, Mbarawa, alisema ofisi hiyo itazipatia ufumbuzi kero na changamoto zinazokwamisha kasi ya kukua kwa biashara katika ushoroba wa Dar es Salaam.

Katika hafla hiyo iliyohudhuriwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi na Miundombinu ya Zimbabwe, Joy Makumbe, Profesa Mbarawa alitaja faida ya kufunguliwa kwa ofisi hiyo kuwa ni kutumia fursa za kiuchumi zilizopo kwa manufaa ya raia wa nchi hizo, kuiweka TPA karibu zaidi na wateja, kuwezesha biashara inafanyika kwa ufanisi kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema Serikali ya Tanzania kupitia TPA, imejipanga kuongeza mchango wa Sekta ya Bandari kukuza pato la taifa kwa kuyafikia masoko yaliyopo nchini humo na kutoa huduma za viwango vya juu vya ubora ili kuhimili ushindani na kuzifanya Bandari za Tanzania kuwa chaguo sahihi kwa wasafirishaji ukanda wa Kusini mwa Afrika.

Akizungumza katika hafla hiyo, Makumbe, alisema kuna ongezeko kubwa la biashara kati ya Tanzania na Zimbabwe katika sekta ya biashara ya usafirishaji magari kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema hali inailazimu serikali yao kuchukua hatua za makusudi za kusimamia ustawi wa biashara hiyo kwa kuondoa changamoto zilizopo.

Awali, Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Juma Kijavara, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, alisema soko la Zimbabwe lina umuhimu mkubwa na imejipanga kuelekeza nguvu kutafuta na kuzitumia fursa zilizopo katika biashara ya usafirishaji magari na shehena nyingine kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Kijavara, alisema TPA inaishukuru serikali kwa kufanya uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Bandari na kuiwezesha kukua kwa kasi kutokana na ufanisi mkubwa wa huduma ya bandari zote nchini.

Hata hivyo, alisema wanafanya maboresho makubwa katika miundombinu ya bandari zao kwa kununua vifaa vya kisasa, kufanya kampeni za masoko za kitaifa na kimataifa, kufanya kazi bega kwa bega na wadau wao.

"Juhudi hizi zimeleta mapinduzi makubwa na matokeo yake ni ongezeko la shehena ya mizigo na mapato ya TPA, sababu inayotufanya kuelekeza nguvu zetu kuyafikia masoko ya nchi jirani ambayo tafiti zinaonyesha zipo fursa za kukuza zaidi wigo wa biashara yetu na mapato yetu," alisema Kijavala.

Akizungumzia kuhusu mpango wao katika mwaka wa fedha 2023/2024, alisema TPA inaanza utekelezaji wa miradi mipya ya upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam kwa kujenga gati namba 12 hadi gati namba 15.

Alisema pia ina lengo la kutumia eneo lililokuwa likimilikiwa na Mamlaka ya EPZA kwa kujenga yadi kubwa ya kuhifadhia magari, maghala na miundombinu ya vyumba maalumu vyenye majokofu ya kuhifadhia bidhaa zinazoharibika haraka.

Balozi wa Tanzania Zimbabwe, Inspekta Jenerali Mstaafu wa Polisi (IGP), Simon Sirro, alisema Jumuiya ya Wafanyabiashara nchini humo imeridhishwa na huduma za Bandari ya Dar es Salaam kwa nchi yao na kuitaka TPA kufanya kazi bega kwa bega na ofisi yake ili kuwezesha Diplomasia ya Uchumi kufanyika kwa ufanisi na kutoa matunda yanayotarajiwa kwa wadau wote wa nchi hizo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mnaopewa kazi kusimamia miradi onesheni uzalendo

**HIVI** karibuni wakati viongozi wa kiserikali wakitembelea miradi ya ujenzi wa majengo ya kutoa huduma kwa wananchi, walibaini kuwapo na tatizo kubwa la ujenzi wa majengo hayo kuwa chini ya kiwango.

Ilibainika kuwa majengo hayo kabla hata ya kuanza kutumika tayari yameanza kuonesha kasoro kutokana na vifaa vilivyotumika kutokidhi viwango.

Katika baadhi ya majengo kulikutwa baadhi ya kuta tayari zimeanza kuweka nyufa, vitasa vya milango vikiwa vimeanza kubomoka na mbao zilizowekwa kwenye kenchi kuanza kuliwa na mchwa na nyingine zikianza kuporomoka.

Ukiangalia thamani ya fedha iliyowekwa kwenye miradi hiyo na ujenzi uliofanyika ni vitu viwili tofauti, huku watu waliopewa kazi ya kusimamia miradi hiyo wakiangalia bila kuchukua hatua zozote.

Inasikitisha kuona mtu anapewa jukumu la kusimamia kazi ili iweze kwenda na thamani ya fedha, lakini anaangalia na kuona kasoro bila kuchukua hatua mpaka kiongozi mkubwa anapopita anaanza kujitetea kwa kujigongagonga.

Kuna miradi kama ya majengo ya vituo vya afya ambayo yanatakiwa kuwa imara ili yasilete madhara kwa wananchi wanaokwenda kupata huduma.

Hata hivyo, miradi hiyo ndiyo inayolipuliwa na kusababisha hata kabla haijakamilika kuanza kuonesha kasoro.

Hivi karibuni Mbunge wa Jimbo la Bariadi alifanya ziara ya kutembelea jimbo lake na kukagua baadhi ya miradi ambayo aliiombea fedha bungeni kutimiza ahadi alizotoa kwa wananchi wake wakati akiomba kura na kubaini kuwa kituo cha afya kilichokuwa kikijengwa kwenye jimbo hilo kujengwa chini ya kiwango na kusababisha sehemu ya jengo hilo kuanza kubomoka.

Kituo hicho cha afya ambacho kiligharimu zaidi ya Sh. milioni 500 kinadaiwa kuwa kenchi zilizotumika kwa ajili ya kuezekea zimeanza kuliwa na mchwa na kuanza kushuka kiasi kwamba zinaweza kusababisha madhara kwa wananchi wanaokwenda kupata huduma.

Wakati serikali ikijitahidi kumaliza kero za wananchi wake zikiwamo za upatikanaji wa huduma za afya, maji, elimu na umeme bado kuna watu ambao wamejivua uzalendo na kuzitumia fedha hizo kwa manufaa yao.

Fedha zinazotolewa kwenye miradi ni nyingi lakini thamani ya vifaa vinavyonunuliwa kufanikisha miradi hiyo haifanani kabisa.

Kazi waliyopewa wasimamizi kuona kama thamani halisi ya fedha ndiyo iliyotumika kununulia vifaa haionekani.

Haileti picha nzuri kama kuna watu waliopewa majukumu ya kusimamia miradi hiyo na wanapoulizwa wanatoa majibu yasiyoridhisha.

Ni vizuri pia miradi hiyo inapoanza utekelezaji wawepo wataalamu wa kuangalia kama thamani ya miradi hiyo inaendana na vifaa vinavyonunuliwa.


Vile vile, wataalamu wanapotoa ushauri ni lazima ushauri wao uzingatiwe ili miradi hiyo iweze kwenda kama ilivyopangwa.

Kanuni ya 114(b), (c) na (d) ya ununuzi wa umma, 2013, inataka taasisi kusimamia ununuzi wa bidhaa, huduma au kazi yoyote inayofanywa na itafuatilia maendeleo ya ukamilishaji wa masharti ya kila mkataba.

Kadhalika, inataka kuchukua au kuanzisha hatua za kurekebisha au kuadhibu ukiukwaji wa masharti ya mkataba na kuhakikisha kwamba majukumu yaliyowekwa na mkataba yanatekelezwa kikamilifu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Utupaji dawa kiholela unaleta hatari ya afya jamii, mazingira

**TUKO** katika zama maendeleo yetu yamepiga hatua, kulinganisha na tulikotoka. Dhana dawa za kisasa zinazopatikana madukani, pia kwa matumizi yake yako juu.

Vilevile kwa sasa siyo ngeni kwa jamii na hata baadhi yetu wamekuwa 'madaktari', wanaojitibu, ingawaje kiuhalisia ni kosa kubwa. Kurejea taifa lilikotoka, ilikuwa gizani zaidi.

Watu wengi waliamini katika dawa za asili na hata tiba ya wakati ule haikuwa katika ufanisi wa sasa. Ngazi ya uelewa ulioko leo ni wa juu zaidi na katika jamii zetu, tukazungukwa na madaktari wa tiba, tunaona namna maduka ya dawa yalivyomea mitaani, ngazi ya kila mtaa mijini.

Utashi na maisha hayo katika tafsiri ya kitaaluma, ndio tunayoita usomi. Nao ukizaa yake mapya ya upande wa pili, yakibeba tafsiri au ujumbe wa uzembe, hasa pale dawa zinapotupwa ovyo mitaani au kukiuka vigezo na masharti ya matabibu wetu.

Shida kuu inatajwa ni jamii ndani ya 'usomi' wao kukosa elimu sahihi katika matumizi, hata hifadhi ya dawa hizo. Dawa zinapotupwa kiholela, inachangia kuzagaa ovyo, ikiwa hatari nyingine.

Inawezekana mtu akaumwa, anaenda hospitali akapatiwa dawa, lakini anapozitumia na kisha kupona, huku akiona kuna dawa zimebaki, anaamua kuzitupa bila kumalizia dozi aliyopewa.

Wapo ambao wanazitupa chooni au katika majalala wanapoona dawa zimebaki, anaridhika wanapojihisi kupona, huku dawa zimebaki.

Hivi karibuni Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Nchini (TMDA) Kanda ya Mashariki imetoa tahadhari kwa wananchi juu ya utupaji holela wa dawa zinazobaki majumbani, kutokana na hatari zake kwa afya ya binadamu na mazingira.

Mkaguzi wa Dawa Kanda ya Mashariki, Japhet Said, anatamka wakati akitoa elimu katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Bibi Titi Mohamed, iliyopo katika Halmashauri ya Rufiji Mkoa wa Pwani.

Akafafanua kwamba, dawa zinazobaki majumbani hazipaswi kutupwa jalalani, chooni, au kwenye vyombo vya kukusanya taka au kuchomwa moto katika maeneo ya wazi, badala yake zirudishwe kwenye vituo vya kutoa huduma za afya vya serikali au ofisi za TMDA zilizopo jirani.

" Dawa zinapotupwa jalalani au kwenye vyombo vya kukusanya taka, watu wasio waaminifu wanaweza kuziokota, wakazisafisha na kuziweka lebo za kughushi na kisha kuzirudisha mtaani ziendelee kutumika hata baada ya kwisha muda wake wa matumizi," anadokeza athari mojawapo.

Katika hilo ana ufafanuzi wa kitaalamu kuwa, dawa hizo ni kemikali ambazo zikibebwa na maji zinapelekwa mbali, hivyo maji yanachafuka, athari inahamia kwa viumbe wa majini wanaoliwa na binadamu, kitu kinachoweza kusababisha magonjwa mbalimbali.

Anaongeza kuwa dawa zilizokwisha muda wa matumizi yake, pale zinapochomwa kwenye eneo la wazi, huzalisha kemikali mbalimbali zinazochafua hewa, hivyo binadamu jirani wanaovuta hewa hiyo wanaweza kuathirika, ikiwamo kupata matatizo ya kupumua, saratani ya mapafu na madhara mengineyo.

Anaongeza kuwa hata ukitupa dawa kwenye shimo la choo bado kemikali zilizomo zinaweza kuua vijidudu vinavyosaidia kinyesi kuoza vizuri na hivyo kusababisha vyoo kutoa harufu kali.

Ni elimu inayofukua wajibu wetu umma, kwamba wananchi wanatakiwa kuacha kufanya hivyo, badala yake wazikusanye dawa zilizobaki majumbani, kwa sababu yoyote ile na kisha wazipeleke kwenye vituo vya afya vya serikali.

Jambo muhimu hapo, ni kwa ofisi za TMDA zilizopo karibu walio jirani nayo kuwawasilishia, nao wanakuwa katika uamuzi wa busara kuzifikisha na wakaziharibu katika njia za kisayansi, zisizo na madhara kwa wanajamii walioko mahali hapo.

Ni jambo jema, namna ufahamu huo ukafikishwa kwa shule 13 za sekondari wilayani Rufiji na kuongeza kuwa wanafunzi na walimu waliopata hiyo elimu waendelee kuisambaza ili kuokoa kizazi cha sasa na kijacho.

Katika hayo ya kawaida, ikiwamo haya yanayohusu afya na mazingira, suala la maisha ya baadaye tuna asilimia kubwa ya namna ya kuyatengeneza kwa namna tunavyoishi.

# TANROADS Bagamoyo yajiandaa na El-Nino

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

KUTOKANA na taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) ya uwapo wa mvua ya El-Nino nchini na Mkoa wa Pwani ukitajwa kuchukua tahadhari mapema, Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), mkoani hapa umeanza kufukua na kufanya ukarabati wa madaraja yaliyoziba.

Meneja wa TANROADS mkoa wa Pwani, Mhandisi Baraka Mwambage, baada ya kufanya ukaguzi wa madaraja na makalavati katika Wilaya ya Bagamoyo na Rufiji amesema wanachukua tahadhari hususani ya mvua hiyo inayotabiriwa kuanza kunyesha mwezi huu (Oktoba).

Mhandisi Mwambage, alisema wakala huo umefanya ukaguzi katika madaraja yote ya Mkoa wa Pwani 318 na makalavati 1,540 kwa kuanza ukarabati, na kuyafukua yaliyoziba.

Vilevile, alibainisha kwamba kati ya madaraja 318 yaliokaguliwa ni 20 ndio yalibainika kuwa na tatizo na yamefukuliwa huku baadhi yakifanyiwa matengenezo ikiwamo daraja la Lukigura lililopo mpakani mwa Mkoa wa Pwani na Morogoro kupitia wilaya za Bagamoyo na Mvomero.

Alisema baada ya kupata taarifa kuhusu tahadhari ya mvua ya El-Nino, walifanya ukaguzi katika madaraja na makalavati kama hatua za awali ambayo ililenga kujua uharibifu ulivyo wa miundombinu na walianza kufanya matengenezo kinga daraja la Mto Ngerengere na wanaendelea.

Kwa mujibu wa Mhandishi Mwambage, matengenezo kinga yanafanyika pia katika daraja la Mazizi, Chalinze Mzee, Kimange, Mkombezi na madaraja madogo yaliyopo upande wa eneo la Manga.

Kadhalika, alisema mwaka 2015 baadhi ya madaraja ikiwamo la Mazizi, lilijaa na kufunga barabara na kwamba matengenezo hayo ni hatua muhimu za awali za kuzuia mafuriko, na aliwatahadharisha wananchi na watumiaji wa barabara ikiwamo madereva kuchukua tahadhari kipindi cha mvua hizo.

Katika hatua nyingine Mhandishi Mwambage, alisema, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Sh. bilioni 18.980 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na madaraja katika mkoa huo na mgawanyo huo Sh. milioni 950 ni kwa ajili ya matengenezo ya madaraja 318 na makalavati 1,540.

**Wakala huo umefanya ukaguzi katika madaraja yote ya Mkoa wa Pwani 318 na makalavati 1,540 kwa kuanza ukarabati, na kuyafukua yaliyoziba.**




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya CPS Africa, Sebastian Dietzold, akitoa mada kuhusu uwezeshaji wa teknolojia ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu kwa kutumia mbao, ambao tayari umeanza kwenye mji wa Fumba Zanzibar, wakati wa mdahalo uliofanyika kwenye maonyesho ya ujenzi ya Dar Construction & Building and CEO Summit 2023, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kulia ni mwongoza mada, Sebastian Kolowa. P**ICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NECTA kupanda zaidi ya miti 100,000 utunzaji mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Mitihani la Tanzania (NECTA) ambao ni wadau wakubwa wa kutumia miti na kararasi zinazotumika kwenye mitihani, limesema litapanda miti 100,700 kuhamasisha utunzaji mazingira.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Mohamed, alisema kuwa miti hiyo itapandwa katika shule zote za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu ngazi ya cheti na diploma ifikapo Desemba, mwaka huu.

Dk. Mohamed aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi katika Shule ya Sekondari Mufindi, mkoani Iringa, wakati akizindua upandaji wa miti kuelekea maadhimisho ya miaka 50 ya baraza hilo.

"NECTA ni miongoni mwa taasisi zinazotumia zaidi karatasi nchini. Tunasimamia upimaji wa darasa la nne, kidato cha pili, mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, kidato cha nne, kidato cha sita na ualimu ngazi ya cheti na diploma.

"Kwa kuangalia takwimu tangu mwaka 1973 hadi mwaka huu, NECTA imetumia karatasi nyingi. Kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2018 hadi 2023 tuna takribani ya watahiniwa zaidi ya milioni 24.

"Watahiniwa hawa kama ni darasa la saba, mmoja anafanya mtihani kwa masomo sita na kila mtihani unakuwa na karatasi ngapi? Karatasi za majibu ngapi? Ukijumuisha utaona NECTA ni watumiaji wakubwa wa karatasi," alisisitiza.

Dk. Mohamed alisema kila Sensa ya Watu na Makazi inapofanyika huonyesha kuwapo na ongezeko la watu. Mwaka 2012 idadi ya Watanzania ilikuwa milioni 44 na mwaka jana imeongezeka hadi kufikia milioni 61.7.

Alisema idadi ya watu inapoongezeka maana yake kuna ongezeko la watahiniwa, hivyo ni lazima baraza lifikirie mipango ya maendeleo ya kiteknolojia ya kuboresha huduma.

Alisema matumizi ya karatasi kwa miaka 40 iliyopita takwimu zinaonyesha, kidunia yameongezeka kwa zaidi ya asilimia 400 na kila siku duniani zaidi ya miti milioni mbili inakatwa.

"Tumeona kupitia maadhimisho ya miaka 50 tangu kuanzisha kwa NECTA na kama watumiaji wakubwa wa zao la miti na karatasi, basi tuwaombe wadau katika vituo vyetu vya mitihani, katika shule zetu za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu ngazi ya cheti na diploma tushiriki kupanda miti na kuisimamia," alisema.

Dk. Mohamed alisema maadhimisho hayo yatakwenda sambamba na kufanyika kwa kongamano la kitaaluma Novemba 29, mwaka huu, visiwani Zanzibar na kuandikwa kwa kitabu cha historia ya Baraza na kufanya maonyesho katika viwanja vya Mnazi Mmoja kuanzia Novemba 30 hadi Desemba 3, mwaka huu na kilele kitakuwa Desemba 4, mwaka huu.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# Waziri Biteko afurahishwa uwekezaji wa bilioni 62/-

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko, amesema uwekezaji wa Dola za Marekani milioni 25 (sawa na Sh. bilioni 62) uliofanywa na Kampuni ya ALAF Limited, ni kutokana na jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji.

Amesema kwa sasa kuna mazingira bora na rafiki kwa wawekezaji kufanya biashara kwa uhuru zaidi ndio maana kampuni hiyo imewekeza kwenye mradi wa mabati ya rangi unaolenga kuokoa dola 190 kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Akizungumza katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi, Naibu Waziri Mkuu huyo ambaye ni Waziri wa Nishati, alisema; "Hili ni jambo la kupongezwa kwasababu inaonesha dhamira ya dhati mliyonayo ALAF limited katika kumthamini Mtanzania kwa kuwafanya kuwa kipaumbele chenu, kuwapa kilicho bora kwa maendeleo ya familia, miji na taifa kwa ujumla."

"Uwekezaji wa namna hii ni wa kupigiwa chapuo kwa kuwa unawekezwa Tanzania kwa manufaa ya Watanzania," alisema.

Alisema uwekezaji huo unaonesha ni kwa namna gani sekta ya viwanda hasa uzalishaji na uongezaji wa thamani unavyokuwa kwa kasi.

Alisema pia uwekezaji huo unatoa taswira njema ya Tanzania ijayo namna itakavyokuwa shindani katika soko la ndani na la nje huku Tanzania ikipunguza utegemezi wa bidhaa za nje kunakotokana na kutotosheleza kwa bidhaa za ndani.

Dk. Biteko alitoa changamoto kwa wadau wengine wa sekta ya uzalishaji wa mabati kuamka na kuwekeza kwa ukubwa, ushindani utatoa faida kwa mlaji kwa kupata bidhaa bora kwa gharama nafuu.

"Nimedokezwa hapa teknolojia itakayotumika hapa ni ya kisasa sana Afrika na hata duniani. Jambo hili linatuhakikishia upatikanaji wa bidhaa bora na za kisasa zaidi, zitakazozalishwa kwa ufanisi mkubwa, gharama kidogo. Hatua hii itatuhakikishia uchumi endelevu na nguvu ya ushindani kwenye masoko ya kimataifa," alisema.

Naibu Waziri Mkuu pia alibainisha kuwa baada ya kukamilika kwa mradi huo, ALAF itatengeneza na kusambaza bidhaa zingine za karatasi zinazotumika kwenye miradi ya ujenzi ambazo alisema zitanakshiwa kwa rangi kupitia mradi huo na kuokoa fedha nyingi za kigeni.

"Nimetaarifiwa ya kuwa, kwa kutengeneza bidhaa hii ndani hapa nchini, taifa linatarajiwa kuokoa fedha za kigeni zenye thamani ya zaidi ya dola milioni 190 katika kipindi cha miaka mitano ijayo ambazo zingetumika kuagiza bidhaa hizo nje ya nchi," alisema Dk. Biteko.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa ALAF Limited, Ashish Mistry, alisema mradi huo utazalisha ajira za moja kwa moja 30 na 250 zisizo za moja kwa moja.

Alisema mradi huo unaokadiriwa kugharimu dola milioni 25 na ambao uzalishaji wake kibiashara unatarajiwa kuanza Desemba 2024, unalenga kuimarisha miundombinu ya kiwanda kilichoko sasa ili kiwe na mwonekano wa kisasa.

Alisema mradi pia umelenga kutoa huduma za kuweka nakshi ya rangi kwa bidhaa za chuma zikiwamo zinazotumika kwenye vyombo vya majini kwa kuzingatia changamoto za kimazingira yaliyoko maeneo ya Pwani ya Tanzania.

# Polisi, wanahabari wakubaliana kuwajibika pamoja

**Na Beatrice Moses**

JESHI la Polisi na waandishi wa habari wameingia makubaliano yanayolenga kuwajibika kwa pamoja kwa maslahi ya nchi, kuepuka migogoro inayochochea uhusiano mbaya wa kikazi kati yao.

Makubaliano hayo yamewekwa juzi kwenye mdahalo uliohusisha polisi na waandishi wa habari uliolenga kuzungumzia usalama wa waandishi, uliofanyika Dar es Salaam, ulioratibiwa na Klabu ya Waandishi wa Habari wa Dar es Salaam (DCPC).

Baadhi ya makubaliano yaliyofikiwa ni kuwa na uzalendo kwanza katika kuwajibika kwao, kuelewa na kuheshimu majukumu ya polisi na waandishi wa habari kwa kuheshimu sheria na katiba ya nchi.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), David Misime, akizungumza kwenye mdahalo huo kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Camillius Wambura, alisema kuna umuhimu kuwapo kwa ushirikiano mzuri baina ya waandishi na polisi kwa kuwa wote wapo kwa maslahi ya wananchi.

"Ni jambo la kusikitisha inapotokea kukosekana kwa maelewano mazuri baina yetu, ingawa inaweza kuwa inachangiwa kwa kiasi kikubwa na malezi ya kifamilia zaidi, kwa kuwa kila mmoja wetu anatambua wajibu wa kazi yake, wakati mwingine siyo kwamba tunakataa kutoa taarifa bali kunakuwa na sababu za msingi zinazotulazimu tuelewane," alisema.

Ofisa wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Victor Maleko, alisema taarifa za matukio ya kufanyiwa ukatili waandishi wa habari zimerekodiwa na taasisi kadhaa ikiwamo UTPC na Baraza la Habari Tanzania (MCT), na katika matukio hayo yapo ambayo yamesababishwa na mgogoro wa maslahi binafsi.



Wafanyabiashara wanaotuhumiwa na makosa sita ikiwamo ya kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya Sh. milioni 592.3 kwa kutoa risiti feki za mashine ya kielektroniki (EFD), wakiwa chini ya ulinzi wa askari kanzu (kushoto), baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala Kinyerezi Dar es Salaam juzi, kusomewa mashtaka yanayowakabili. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Kortini madai kuisababishia TRA hasara mil. 592/-

**Na Grace Gurisha**

WAFANYABIASHARA wanne wa Dar es Salaam, wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, wakikabiliwa na mashtaka sita ikiwamo ya kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya Sh. milioni 592.3 kwa kutoa risiti feki za mashine ya kielektroniki (EFD).

Washtakiwa hao ni Salum Mbegu (38), mkazi wa Majohe Mji Mpya, Peter Ntikula (27), mkazi wa Buguruni, Baraka Ntikula (37), mkazi wa Mkuranga na Hamad Hamad.

Walisomewa mashtaka yao na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Gloria Mwenda akisaidiana na Upendo Mono, Medalakini Emmanuel na Hauni Chilamula, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Susan Kihawa.

Mwenda alidai washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka ya kuongoza genge la uhalifu, kutumia mashine za kielektroniki (EFD) kwa lengo la kuharibu mfumo na kumdanganya Kamishna, kutoa risiti zisizo halali za EFD, kukutwa na mali iliyoibwa au kupatikana kinyume na sheria, kuisababishia mamlaka hiyo hasara na kutakatisha fedha.

Alidai kuwa katika shtaka la kwanza inadaiwa kati ya mwaka 2018 na Oktoba 3, mwaka huu, maeneo ya Buguruni Kisiwani, wilayani Ilala, Dar es Salaam, kwa lengo la kujipatia faida, waliongoza genge la uhalifu kwa kutumia mashine ya EFD kuharibu mfumo, kumdanganya Kamishna na kutoa risiti zisizo halali.

Pia, alidai katika tarehe hizo, washtakiwa hao walitumia mashine za EFD kwa lengo la kupotosha mfumo kwa kutoa risiti zisizo halali na kuziingiza kwenye mfumo wa TRA na kusababisha mamlaka hiyo kudaiwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya Sh. 592,336,714.

Ilidaiwa washtakiwa hao kwa pamoja walitoa risiti bandia za EFD kwa nia ya kumdanganya Kamishna na walipa kodi kudai VAT kinyume na sheria.

Katika la shtaka la nne inadaiwa Oktoba 3, mwaka huu washtakiwa Mbegu, Ntiluka na Baraka, walikutwa na mashine tano za EFD ambazo walizipata kinyume na sheria. Inadaiwa kati ya mwaka 2018 na Oktoba 3, mwaka huu, washtakiwa hao kwa pamoja waliisababishia TRA hasara ya Sh. milioni 592.3 kwa kutoa risiti zisizo halali.

Mwenda alidai katika mashtaka ya sita ya utakatishaji fedha, washtakiwa hao kwa pamoja walihusika kutoa muamala wa Sh. milioni 592.3 wakati wakijua fedha hizo kuwa zao la genge la uhalifu.

Washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo na upande wa mshtaka ulidai kuwa upelelezi bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.





# Waliopitia mafunzo JKT Oljoro wachangisha mil.16/-

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WALIOWAHI kupitia mafunzo ya kujitolea ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kikosi cha Oljoro, wamechangisha zaidi ya Sh.milioni 16.7, kwa ajili ya kufadhili ujenzi wa jengo la kituo cha watoto yatima cha Habashabi kilichopo Kisongo wilayani Arusha.

Jengo hilo litakuwa mahususi kwa ajili ya kusomea na kutoa huduma ya maombi.

Akizungumza jana jijini Arusha, wakati wa hafla fupi ya kuwakabidhi eneo hilo, mtoa huduma kwa jamii, Kanda ya Kaskazini wa Chama cha Marafiki Waliohitimu Mafunzo ya Kijeshi ya JKT (MAO), Festo Msofe, alisema chama hicho kilichoanzishwa mwaka 2015, kimekusanya fedha hizo kupitia kundi sogozi la WhatsApp.

MAO ambayo inajumuisha waliopata mafunzo JKT Oljoro, kati ya mwaka 1991/1992, malengo yake ni kusaidiana na kusaidia jamii inayowazunguka ikiwamo yatima.

Aidha, chama hicho kimetoa msaada wa vyakula, vinywaji, nguo na vitu mbalimbali kwa watoto yatima wa kituo hicho.

"Tuliunda group la WhatsApp tukaanza kuchanga ada kila mwezi na kila mwaka tunatoa msaada kwenye eneo tunalolipendekeza, kama hapa kwenye kituo hiki tulikuja mwaka 2021 tukaona wanauhitaji wa eneo hili tukaanza kuchangishana na leo tumetimiza ndoto yetu.

Akifafanua zaidi kuhusu misaada hiyo, Katibu wa MAO, Frida Mlingi, alisema mwaka 2021, walipofika kituoni hapo kwa mara ya kwanza, waliwanunulia watoto bima za afya, vyakula na mwaka huu wamechangishana fedha.

Mwakilishi wa watoto yatima katika kituo hicho, Jackline Jeremia, aliishukuru MAO kwa misaada yao, ukiwamo wa kuezeka eneo hilo ambalo wanalotumia kusoma na kuendeshea maombi.

"Licha ya kutusaidia bado tunakabiliwa na ukosefu wa fedha za kuendeshea kituo, kulipia ankara za maji, umeme na uwezo mdogo wa kulipa ada za shule.

...Tuna shida nyingine ya ukosefu wa bima za kudumu, lakini tunahitaji kingamaji na tangi la kuhifadhia maji kwa kuwa eneo hili upatikanaji wa maji ni wa shida," alisema.

Mkuu wa kituo hicho, Leticia Julius, alisema kituo hicho kilianza mwaka 2015 na hadi sasa kina watoto 27 ambao kati yao, 16 wapo shule ya sekondari, sita msingi, wanne vyuo vya kati na mmoja amehitimu kidato cha sita.

# Watoto wa chekechea wapewa msaada wa madawati 200

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

**Baadhi ya shule katika halmashauri hiyo wanayo madawati hayo licha ya kwamba wanatakiwa kukalia mikeka kwa kuwa wanajifunza kwa vitendo.**

SHIRIKA la World Vision Tanzania (WVT), limewezesha upatikanaji wa madawati maalumu 200 katika Mkoa wa Manyara kwa ajili ya watoto wa elimu ya awali.

Jana, Ofisa Elimu wa WVT, Akaunsia Munuo katika mahojiano yake na Nipashe, alisema wameamua kufadhili ununuzi wa madawati hayo kwa kuwa madarasa mengi ya elimu ya awali katika mkoa huo hayana sifa kwa ajili ya kutoa elimu ya awali.

Alisema tatizo hilo la kukosekana madawati maalumu ya darasa la awali yenye sifa linatajwa kuathiri mchakato wa utoaji wa elimu ya awali, ambayo pamoja na mambo mengine inamwandaa mtoto kuanza darasa la kwanza.

Katika shule nyingi za msingi ambazo ndizo zinapaswa kusimamia elimu hiyo, miundombinu ya utoaji wa elimu hiyo inasikitisha.

Kwa mujibu wa Munuo watoto hao wa darasa la awali wanatakiwa kuwa na madawati maalumu ili wakikaa darasani wasining'inie kwenye madawati.

Alisema kitaalamu wanafunzi wakining'iniza miguu wanashindwa kusoma vizuri na wanakosa uhuru wa kumsikiliza mwalimu.

Aidha alisema ili kuhakikisha watoto hao wanawajengea uwezo walimu wao ambao wanasaidia kuwafundisha makuzi ya mwili, kihisia na kijamii, lugha na watoto huwapatia vifaa vya michezo ili visaidie mazingira ya darasani kumvutia mtoto ajifunze kwa vitendo.

Ofisa huyo alisema pia wamesaidia kwa watoto hao vifaa vya kujifunzia ikiwamo midoli na vibao vya kuandikia.

Kwa upande wake, mtaalamu wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC), Davis Gisuka, akizungumzia umuhimu wa madawati maalumu ya wanafunzi wa awali, alisema wanafunzi wa awali wanahitaji samani ambazo zinaendana na umri wao.

Gisuka alieleza kuwa madawati yanatakiwa yawe na nafasi ili wakiambiwa kusimama waweze simama haraka.

Aliyataja madhara ambayo yanaweza kujitokeza watoto hao wakikalia madawati yasiyoendana na umri kuwa ni miguu kwamba wakikaa itaning'inia na kuvimba na kusababisha damu kutotembea kwenye mishipa.

Licha ya kueleza kuwa watoto hao wanatakiwa kukalia madawati maalumu, mtaalamu huyo alisema wao katika maeneo wanayotoa elimu ya awali wanafunzi hao wanapaswa wakae kwenye mikeka na mazuria kwa kuwa mikeka inawasaidia kutembea haraka pindi wanapoitwa.

Gisuka alisema Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 inaeleza kuwa kila mwalimu mmoja wa awali anatakiwa afundishe wanafunzi 25 na awe na msaidizi wake.

Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Simon Mumbee, alisema katika makuzi ya watoto yanatofautiana hivyo wakiwekewa madawati makubwa watashindwa kukaa lakini madawati maalumu yanawasaidia kuandika vizuri.

Vilevile, alisema baadhi ya shule katika halmashauri hiyo wanayo madawati hayo licha ya kwamba wanatakiwa kukalia mikeka kwa kuwa wanajifunza kwa vitendo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Anna Mbogo, akimvisha viatu mtoto wa Shule ya Msingi Gallapo, vilivyotolewa na Taasisi ya Mama Ongea na Mwanao inayoendesha kampeni ya Samia Nivishe Viatu juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# OSHA yaanzisha kampeni ya upimaji magonjwa kazini

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (OSHA), imeanzisha kampeni ya upimaji wa magonjwa yatokanayo na kazi, ili kuwasukuma wakuu wa idara za utawala na rasilimali watu katika utumishi wa umma kutambua kuwa hilo ni jukumu la kisheria na sio takwa la mwajiri.

Kutokana na umuhimu huo, Ofisa Mafunzo wa OSHA, Simon Lwaho, amewataka wakuu hao wa idara kushirikiana na wakala huyo kuimarisha mifumo ya usimamizi wa masuala ya usalama na afya katika maeneo yao ya kazi ili kuleta tija kwa taifa.

Lwaho, alikuwa akizungumza jana jijini Arusha baada ya kuwasilisha mada kuhusu masuala ya usalama na afya mahali pa kazi na takwa la kisheria la upimaji wa magonjwa yatokanayo na kazi.

Katika kikao hicho, Mkaguzi wa Afya wa OSHA, Amina Nangu, alisema wakuu wa idara za utawala, ndiyo watoa maamuzi katika maeneo yao ya kazi, hivyo wakielewa vyema sheria na miongozo ya usalama na afya mahali pa kazi wataweza kuisimamia utekelezaji vizuri.

Baadhi ya wakuu wa idara za utawala katika utumishi wa umma kutoka maeneo mbalimbali nchini, wamekiri kuna umuhimu kwa watumishi kutambua hali zao za kiafya, hususani kufanya uchunguzi wa magonjwa yatokanayo na kazi.

Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala katika Manispaa ya Bukoba, Erick Bazompora, alisema kuwa watumishi wanapotambua hali zao za kiafya mapema ni rahisi kujikinga dhidi ya madhara husika.

Kikao kazi hicho, kilifunguliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Boniface Simbachawene.



# RC atoa siku 30 halmashauri kumlipa kikongwe mil.22/-

**Na Vitus Audax,** ILEMELA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, ametoa muda wa mwezi mmoja kwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kumlipa fidia ya Sh. milioni 22 kikongwe Rahel Mkoma aliyetoa eneo na kupisha ujenzi wa Shule ya Bujingwa katika halmashauri hiyo.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa mkutano wake wa kusikiliza kero za wananchi ambao ulifanyika kwenye viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilemela kwa zaidi ya saa nane.

Alisema ni haki ya bibi huyo kilipwa fidia yake ya Sh.milioni 22 kama sehemu ya fidia ya ardhi aliyoiachia kwa ajili ya mradi wa jamii mwaka 2016 na kuitaka halmashauri hiyo kufanya malipo hayo ifikapo Novemba mwaka huu.

**Hatuwezi kuwa tunasikiliza kero kila mara tunasema na wewe ulipwe na wewe ulipwe fanyeni uhakiki walipwe fidia zao.**

"Wapo wananchi wengi wakiombwa na serikali maeneo kwa ajili ya miradi ya maendeleo wanatii lakini nimebaini kuwa wanacheleweshewa kulipwa fidia zao, hivyo nakuagiza Meya nendeni mkahakiki madeni yote wanayodai wananchi ya fidia. Hatuwezi kuwa tunasikiliza kero kila mara tunasema na wewe ulipwe na wewe ulipwe fanyeni uhakiki walipwe fidia zao," alieleza Makalla.

Katika mkutano huo, Makalla alipokea kero mbalimbali nyingi zikiwa za ardhi na idara ya ardhi ikishutumiwa kuwa chanzo cha migogoro hiyo kwa utendaji na majibu yanayoelezwa kuwa mabovu kwa wananchi.

Aidha, alitoa siku 14 kwa idara hiyo kuhakikisha inashughulikia kero hizo na kuwasilisha taarifa kwake kuwa zimefanyiwa kazi na kila mwananchi awe amejibiwa.

Kuhusu wananchi waliovamia eneo la upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza, Makalla alisema kuwa ameunda kikosi kazi kitakachofanya tathmini ili kubaini wangapi wanapaswa kupisha upanuzi wa uwanja huo kama hitaji la serikali linavyotaka.

Katika hatua nyingine, Makalla aliwataka wananchi wa Ilemela kuwa watulivu wakati serikali ikikamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji kwenye maeneo yao kufuatia ukamilishaji wa mradi mkubwa wa chanzo cha maji Butimba unaotarajiwa kuzalisha lita milioni 48 kwa siku.

"Mradi wa Maji Butimba ndio tegemeo katika kutatua tatizo la maji, nimekagua mradi huo na maji tayari yameanza kutoka na mabomba yameshasambazwa Ilemela kwa ajili kuwafikia wananchi wote, hivyo msiwe na wasiwasi serikali yenu inafanya jitihada na hivi karibuni tatizo hilo litamalizika," alisema.

Aidha, Makalla alifafanua kuwa katika jitihada za kuhakikisha wananchi wa Mwanza wanapata maji, serikali imetoa fedha zingine kwa ajili ya kufanya marekebisho na upanuzi wa mradi wa sasa wa maji wa Kapripoint ili kuhakikisha wananchi wanapata maji ya kutosha kwa kusaidiana na mradi mpya unaojengwa.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla (kulia), akizungumza katika mkutano wa kusikiliza kero za wananchi katika viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilemela juzi, ikiwa ni mwendelezo wa mikutano yake ya hadhara inayojumuisha wananchi na viongozi wa idara za kila halmashauri. **PICHA: REMMY MOKA/SAUT**

## Mtoto afariki dunia akitumbukia bwawani

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MTOTO Victoria Mhoja (3) mkazi wa Kijiji cha Nyamtelela mkoani Mwanza amefariki dunia baada ya kutumbukia katika bwawa la maji alipokuwa akichota maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Elias Shija alithibitisha kutokea kwa tukio hilo akilitaja kuwa ni la pili kutokea kijijini hapo likitanguliwa na moja lililotokea mwaka 2017.

Alisema mtoto huyo alienda bwawani hapo kuchota maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani Jumamosi majira ya saa 11 jioni ndipo alipoteleza na kutumbukia bwawani.

Mwenyekiti huyo alieleza kuwa kipindi mtoto huyo anaenda kuchota maji wazazi wake walikuwa wameenda kusia mbegu za mpunga shambani na watoto hao walienda bwawani wakiwa peke yao.

Alisema kuwa mtoto huyo alipotumbukia mwenzake alirudi nyumbani analia na kwenda kumweleza babu yake ndipo wakaenda kwa Mwenyekiti wa Kitongoji ili atoe taarifa.

Hata hivyo alisema bwawa hilo lilichibwa na makandarasi miaka nane iliyopita wakati wa ujenzi wa barabara na sasa mvua zikinyesha linajaa na kutumika kama kisima.

Shija alisema kwa sasa wanamikakati ya kutengeneza fensi na kuzuia watoto chini ya miaka mitano kufika bwawani hapo.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo waliiomba serikali kuweka uzio kwani bwawa hilo limekuwa tishio na kuhatarisha maisha ya watoto.

Kutokana na tukio hilo, aliwatahadharisha wazazi na walezi wa Kijiji cha Nyamtelela kuwa makini na watoto wao pamoja na kuacha kuwaagiza kwenda kuchota maji katika eneo hilo, huku wakiendelea na mchakato wa kuweka uzio bwawani hapo.

# Naibu Waziri amwaga chozi akidai h/shauri inahujumiwa

**Na Jenesta Jasson,** BUKOBA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Steven Byabato, ametoa machozi mbele ya wananchi wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera akidai halmashauri hiyo inahujumiwa kimaendeleo.

Byabato alimwaga machozi juzi wakati wa uzinduzi wa ukarabati wa mradi Stendi ya Manispaa ya Bukoba ambayo miundombinu yake imekuwa mibovu kwa muda mrefu na kuzorotesha hali ya kimaendeleo katika halmashauri hiyo.

Naibu waziri huyo alionesha kusikitikwa na hujuma zinazofanywa na baadhi ya viongozi ambao hakuwataja ambao wanakwamisha maendeleo katika Manisipaa ya Bukoba, akitolea mfano wa stendi hiyo ambayo imekuwa mbovu kwa muda mrefu.

Alisema licha ya stendi hiyo kujengwa kwa muda mrefu na kutumiwa na mabasi yaendayo mikoani na nje ya nchi, uchakavu wake umekuwa wa muda mrefu huku juhudi za muda mrefu kuifanyia marekebisho zikigonga mwamba.

"Hii stendi ilijengwa kabla ya Uhuru wa Tanganyika, imetumiwa na abiria wengi kuingia na kutoka ndani ya mkoa lakini juhudi za kuikarabati zimekuwa zikihujumiwa na baadhi ya watumishi na kufanya hali kuwa tete hususani kipindi cha mvua ambapo imekuwa haingiliki," alisema Byabato.

Aidha, baadhi ya viongozi wa Manispaa ya Bukoka waliishukuru serikali kwa kutoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo na kutoa ahadi ya kuusimamia kikamilifu.

Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Erasto Sima aliahidi mbele ya wananchi na Naibu Waziri huyo kuusimamia mradi huo na kusimamia fedha zilizotolewa kufanya ukarabati wa mradi huo mpaka kukamilika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Bukoba, Hamidi Njovu alieleza kuwa mradi huo utakavyotekelezwa na kuwatoa wasiwasi wananchi kuwa mradi huo watausimamia na utakamilika kwa muda uliopangwa.


Naye Mstahiki Meya wa Manispaa ya Bukoba, Godson Gibson, alisema kuwa stendi hiyo itatengenezwa kwa viwango vya juu na itasimamiwa ili ikamilike kama ilivyopangwa na kuanza kazi mara moja.

ama
ALHAMISI OKTOBA 19, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

## KIJUE CHAMA KIPYA CHA WAGUMBA
**Waanza safari na ajenda mbili kuu, kutambulika na mabadiliko kisheria**



## ‘NJOO NA MWENZA’ ILIVYOTEGULIWA KLINIKI

Ukurasa 12

# Undani wake Mradi Maji Victoria aliyouzindua Rais Samia Singida

**Na Mwandishi Wetu**

NI wiki ya neema mkoani Singida, ambayo kwa heshima kubwa, umezinduliwa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya Mji wa Shelui, tukio linalotanguliwa na Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mkoa Singida.

Kwa lugha fupi, mkoa wenyewe umezaliwa wastani wa mwaka mmoja, tangu Tanganyika kuwa Jamhuri, 1962.

Aina ya kicheko kama cha wiki hii cha kupata rasmi maji ya Ziwa Victoria, kwa majirani zao mji wa Tinde, Shinyanga kilikuwa Januari mwaka huu.

Kwa yote hayo yaliyotokea Singida, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akawa mgeni rasmi, hafla ya kupata maji ilifanyika kwenye kijiji cha Kizonzo, wilayani Iramba.

Ni zawadi kwa mara nyingine, hata serikali ya Awamu ya Sita inawawezesha wana - Singida kujihisi wanafaidika na maji ya Ziwa Victoria, waliyokuwa wanaishuhudia kwa watangulizi wao mkoa wa Shinyanga.

Kwa mujibu wa Waziri wa Maji. Jumaa Aweso ni mradi uliogharimu Sh. bilioni 24. Tangi la maji lililopo katika kituo hicho kijijini Kizonzo, lina ujazo wa lita 300,000, ikiwa sehemu ya Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya Mji wa Shelui.

Viongozi wengine walioambatana na Rais Dk. Samia, mbali na Waziri Aweso, ni Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwa mbunge wa mkoani Singida na Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Srikanta Pradhan.



Rais Samia Suluhu Hassan, akizindua mradi mkubwa wa maji Ziwa Victoria, eneo la Shelui, Singida, juzi. **PICHA: MTANDAO.**

Rais Dk. Samia, katika halfa hiyo ya maji, akawahakikishia wananchi wa wilayani Mkalama, kuwa suala la upatikanaji majisafi na salama kwao, linaendelea na kufanyiwa kazi na serikali, akiwahakikishia tatizo la maji linaisha kabisa wilayani hapo, kwa kuwa serikali imepeleka fedha za kutekeleza miradi ya maji.

Mbunge wa Mkalama, Francis Isack naye anampongeza na kumshukuru Rais kwa kutoa kiasi cha shilingi bilioni 3.3 kupitia Wizara ya Maji, kuwaletea majisafi na salama, sasa upatikanaji wake ni wa uhakika.

Akasema, kiasi cha shilingi milioni 480, zimetengwa kwa mwaka wa fedha uliopo- 2023/2024, kwa ajili ya kujenga tanki la kuhifadhi maji wilayani Mkalama.

Akizungumza kwenye ziara yake kwenye mradi huo mnamo Januari mwaka jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, akatamka:

“Mradi huu wa Maji wa Tinde mkoani Shinyanga hadi Shelui mkoani Singida umegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 24.6...tunamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha, ili wananchi wake wapate huduma ya majisafi na salama.”

**SAFARI ILIKOANZA**

Mradi ukiwa umeanza miezi kadhaa mnamo Januari 3 mwaka jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Sanga, akaeleza kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo wa majisafi na salama ya Ziwa Victoria, kutoka Tinde wilayani Shinyanga hadi Shelui Singida.

Akabainisha hayo alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi huo katika Mji wa Shelui na Tinde wilayani Shinyanga.

Mwaka mmoja baadaye Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Janauri 19, 2023 akazuru katika mji wa Tinde kuweka jiwe la msingi la Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kwenye Mji wa Tinde.

Wakati huo ikatajwa, ungeharimu shilingi bilioni 5.2 na kunufaisha wananchi 60,000 katika vijiji 22 vya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Akizungumza baada ya kuweka jiwe hilo la msingi Dk. Mpango, akasema ni mradi wa maji katika miji ya Tinde mkoani Shinyanga Shelui, Singida, unakogharimu shilingi bilioni 24.4, kwa matarajio ya kuwafikia wananchi 180,000 wa Tinde, Shelui na vijiji jirani vinavyonufaika na mradi huo.

Dk. Mpango akaviagiza vyombo vya dola, pamoja na Kamati za Ulinzi na Usalama, kuwasaka wote waliojihusisha na wizi wa maji, kuwachukulia hatua kali za kisheria.

“Wapo watu wanachepusha

Inaendelea Uk. 14

AFYA

# ‘NJOO NA MWENZA’ ILIVYOTEGULIWA KLINIKI

- Hoja lazima, ikajibiwa na mume wa kukodi
- Simulizi ya bodaboda anayekimbia vipimo
- Mikasa ya ‘mume wa mtu’; ‘wangu amefariki’

**Na Beatrice Shayo**

KUTAMANI fedha, kukimbia vipimo na kutojua jina la ‘mwenza’ ni mitihani inayowakuta wenza ‘feki’ hasa madereva wa bodaboda wanaoambatana kliniki na wajawazito wasio waume zao.

Dereva bodaboda anayelipwa Sh. 10,000 kwenda kliniki, amevutiwa na fedha bila ya kujua kitakachompata; kutokuwa na taarifa za ‘mkewe’, uzao wa ngapi na maelezo ya mtoto anavyocheza tumboni, ikiambatana na ‘kubwa lao’, kukimbia vipimo vya Virusi vya Ukimwi (VVU).’



Mzazi wa kiume akiwa kliniki na mtoto wake. **PICHA: MAKTABA**

### BODABODA NA VVU

Mwendesha bodaboda Ally Salum, anasimulia abiria alivyomwomba amsindikize kliniki kwa kuwahadaa ni mume wake, akiahidiwa Sh. 10,000, badala ya Sh. 2,000, za usafiri walizokubaliana.

Salum anasimulia kosa walilofanya, mteja hakumpanga vizuri kuhimii maswali tarajiwa, hata bodaboda huyo analazimika kuwa ‘bubu’ wakati fulani, akitafuta majibu.

“Hawakunishtukia, japo nilikuwa najibu kwa kubahatisha. Mtihani ulionikuta ni kuambiwa kufanyiwa kipimo cha Virusi vya Ukimwi (VVU), hapo ndipo nilichoka akili!

“Ikabidi niwe muwazi, ‘huyu ni abiria wangu, aliniomba nije naye hapa kituo cha afya kwa sababu mmemtaka aje na mwenza wake’, baada ya kueleza hayo nikaondoka zangu,” anasema.

### KUTOKA KWA WAUGUZI

Muuguzi wa Hospitali ya Arafa Ugweno, iliyopo Tandika, Dar es Salama, Latifa Masasi, anataja wajawazito wamewafikia na wenza ‘feki’ wakiwamo waendesha bodaboda na ndugu zao.

Anasema, kipimo kinachowafahamisha ni aina ya maswali wanayowauliza wateja, wanashindwa kuyatolea majibu. Latifa anasimulia: “Mfano tumewapa madaftari kwa wale ambao umri wa mimba umeshakuwa labda ana wiki 28 au 32, tunauliza mtoto amecheza kwa siku mara ngapi?

“Tumewapa hayo madaftari, nataka aniambie mtoto wake amecheza mara ngapi asubuhi na usiku anapokwenda kulala amecheza mara ngapi. Hilo swali inabidi nimuulize baba, ‘mtoto wenu’ amecheza mara ngapi... anababaika, hakuambii chochote.

“Hajui masuala ya mtoto kucheza wala nini! Je, VVU kwa pamoja unamuuliza, mlifanya hivyo vipimo? Yaani akishasikia suala la vipimo na akishamleta, tunamwambia tunataka kukupima kujua afya yako na mke wako.

“Endapo kutakuwa na maambukizi, ili mjue namna ya kumkinga mtoto endapo ikitokea mna mamabukizi ukishasema hivyo anatimka,” anasema.

Ndipo anasimulia mkasa mwendesha bajaji anayepaki karibu na kituo chao cha afya, mjamzito alimchukua wakaja naye, kumbe wanafahamiana...

Anasema kutokana na hali hiyo imewabainisha na sasa wanafuatilia kwa umakini maswali anayowapa wagonjwa na yanapofika matatu, hubaini usahihi uliko.

Hapo anatoa mfano hai katika swali, inapotokea upotoshaji, mjamzito hupata majibu ya uamuzi huo ni baada ya kuonekana ucheleweshaji wa kurejea majumbani kwa shughuli zingine.

“Wapo waliorudishwa kwenye vituo vya afya, kisa hawajaenda na wenza wao, wakija hapa kwetu wanaogopa kuvitaja...

“Wanatuambia kule tumeenda, hawataki kunipokea mpaka niwe na mwenza wangu, nimeenda kwingine nimeambiwa hivyo,” anasimulia mjamzito.

Anafafanua kwamba, mjamzito anapobakiza wiki mbili kujifungua, wanawahisha, kwa sababu za kuchelewa kuanza kliniki, wanapata majibu kila kituo walichoenda wamedaiwa kwenda na mwenza.

“...nadhani hakuna haja ya kuacha kumhudumia mjamzito, kisa hajafika na mwenza wake, kwani unazidi kumweka katika hali ya hatari,” anaelimisha muuguzi huyo.

### JITIHADA & BABA BORA

Kwa mujibu wa muuguzi huyo, inapotokea mjamzito anakuwa chini ya wiki 12 anataka kuanza kliniki anarudishwa, kisa hajafika na mwenza wake ni hatari kiafya, hasa ujauzito wake unapokuwa na tatizo.

Hap anataja matatizo kama kukosa damu au shinikizo la damu, kupanda au kushuka, maambukizi ya VVU, vyote anavitaja vinachangia shida kwenye ujauzito.

“Kwa sababu hajaja kupima tangu mwanzo, ukajua uanze vipi kumpa dawa ya kumkinga mtoto, sasa kama utamchelewesha inasababisha mtoto kuzaliwa na maambukizi ya Ukimwi,” anafafanua.

Anataja madhara yake ni kama, kifo cha mama kwa kupungukiwa damu, akiendelea: “Ndio maana kuna baadhi wanakimbilia hospitali binafsi, wakiamini watahudumiwa kwa haraka na bila kusumbuliwa suala la mwenza.”

Anataja faida ya kuanza kliniki mapema, mjamzito anapatiwa elimu kwa hudhurio linalofuata ni kuja na mwenza wao.

“Kila wagonjwa wanavyokuja hata kama anaenda kitengo cha meno au huduma nyingine, huwa tunawajumlisha na kuwapatia elimu ya wajawazito kwa wote, najua ujumbe utafika...

“Baba anapokuja na mke wake, akifika hata kama kuna foleni watu 20, tunaanza na yeye kwanza, ili awahi kwenda kazini,” anakiri kuchangia usumbufu kwa waliowahi klinikii.

Anasema ni kitendo kinacholeta usumbufu kwa wale waliowahi foleni na wanapoona hali hiyo kliniki zinazofuata, wanakuja na wenza wao, ili kupata upendeleo katika foleni.

“Unajua wakati mwingine mwenza wake labda ni mume wa mtu, hawezi kuja naye hapa. Hivyo, anajikuta anatafuta hata bodaboda twende ukaonekane wewe ni mume wangu,” anasema.

Muuguzi Latifa anaeleza wilayani Temeke, kituo chao cha afya kinaongoza kuwa na Baba Bora wanaowasindikiza wake zao kliniki na hata kujinyakulia zawadi kama simu na majiko ya gesi.

Anataja anachokifurahia, kuna Baba Bora zaidi ya 900 hata wameunda kundi lao la mtandao wa simu wakiwa 440, akiwamo mwenyekiti wa serikali za mitaa na ofisa mtendaji wa ajili ya wanaowahamasisha.

### SASA SIO LAZIMA

Mratibu Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto Mkoa wa Dar es Salaam, Agnes Mgaya, anasema sasa sio lazima kwenda na wenza kliniki, ikitengua uamuzi wa awali.

“Wizara inapotoa miongozo kama mkoa tunaitafsiri na kuishusha chini na kuwaeleza mwelekeo,” anasema Agness.

Pia anafafanua kubaini taarifa za wanaodai waume zao wamefariki na kuwaacha wajawazito, wakaona inajenga tafsiri mbaya katika sura adhabu kisaikolojia, anawahi kufika anahudumiwa mwisho.

“Mwingine akaonekana amebakwa bado anafika kliniki hapewi kipaumbele, ikabidi tuwaeleze waiache hiyo...” anasema Agness.

“Tulikuja kupokea malalamiko, unakuta mtu anawahi kufika hapewi huduma. Kwa wakati huku akieleza mume wake, amesafiri kwanini ananyanyapaliwa.

“Tukaona wana hoja ya msingi, ni bora tuache! Kwa hiyo, kutokana na hali wakaona haina haja ya kuhangaika kumtafuta bodaboda...” ananena.

### MFANO HOSPITALINI

Muuguzi Kiongozi wa Kitengo cha RCH (Mama, Baba, Mtoto na Vijana) katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam, Salome Sallu, anasema katika kituo chake hawajawahi kumnyima mjamzito kupata huduma hata kama hajafika na mwenza wake.

“Sijakutana na hiyo kesi, wanakuja na wenza wao tunawafanyia vipimo, lakini akija mtu ambaye hana mwenza wake, huwa hatumrudishi. Nadhani ukisema unamrudisha, mpaka ukamlete mwenza wako, anaweza kuja na kijana yoyote,” anatamka.

“Ukimweleza umuhimu ni kwanini anatakiwa kuja na mwenza wake na kumshauri ajitahidi kumleta, itasaidia, maana tutawachukua vipimo yeye na mwenza, afya yake sio ya kwake, ya kwako. Wakijua umuhimu, watawashawishi waje...,” anatamka.

Michael Mrisho, aliye alifika na mwenza Hospitalini Mnazi Mmoja, anakiri yanayosemwa, kwamba binafsi hajaona changamoto ya kwenda kliniki na inamsaidia kujua afya yake, kutokana na vipimo wanavyofanyiwa.

Anaeleza sababu ya wanaume kutofanya hivyo, inatokana na kubanwa na majukumu na wapo wanaogopa kuhudhuria kliniki.

Michael, anasema siku ya kwanza amekutana na ucheleweshaji kutokana na vipimo walivyotakiwa kufanya, hali inayoweza kuwakatisha tamaa kinababa wasio wavumilivu.

### WAZIRI ASHAURI

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Molel, anasema wajawazito sio lazima kwenda na wenza wao katika vituo vya afya na hairuhusiwi kumnyima huduma kwa kutofika na mwenza wake.

“Tulisema wajawazito wawe wanakuja na wenza wao lengo lilikuwa ni kuwahamasisha kuhudhuria kliniki....,”anasema Dk. Molel.

AFYA

## KIJUE CHAMA KIPYA CHA WAGUMBA

# Waanza safari na ajenda mbili kuu, kutambulika na mabadiliko kisheria



Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Vivian Women Organization Tanzania (VIWOTA), Vivian Ugulumu, akiwafundisha wanafunzi wa Shule ya Sekondari Benjamin Wiliam Mkapa, masuala ya ugumba na madhila ya mapenzi hatarishi pamoja magonjwa yake. **PICHA: BEATRECE PHILEMON**

**Na Beatrice Philemon**

UNAPOZUNGUMZIA ugumba, si watu wote wanaofahamu maana ya neno hilo. Huwa ni pale mtu anapata changamoto ya uzazi, ambazo humfanya ama kupata watoto kwa kuchelewa, wachache au kutojifungua kabisa.

Ugumba unaweza kuwa kwa jinsia zote, mwanamke au mwanaume. Ni kinyume na jamii ilivyozoea kuwa ni shida ya mwanamama pekee.

**SABABU ZAKE**

Kunatajwa ni kufanya mapenzi katika umri mdogo, pia kumeza dawa za uzazi wa mpango katika umri huo, utoaji mimba holela, magonjwa ya zinaa kama kaswende, ngono, matumizi mabaya ya dawa ya kulevya, mapenzi kinyume na maumbile kwa watoto wa kike na kiume.

Pia kuna suala la mfumo mzima wa maisha, msongo wa mawazo uliopitiliza, uvutaji sigara, kunywa pombe kulikopitiliza, kuwa na mbegu dhaifu, kujichua uume kwa muda mrefu, pia aina za vyakula.

Kwa sasa, baada ya kuona watoto wanapitia changamoto nyingi za ukatili wa kijinsia na unyanyasaji, hata kuangukia ugumba, wadau Shirika lisilo la kiserikali la Vivian Women Organization Tanzania (VIWOTA), Chama cha Wagumba Tanzania, kwa kushirikiana na wadau wengine wameanzisha kampeni kuelimisha jamii, wakiwamo wanafunzi kuhusu dhana ya ugumba na visababishi vyake.

Mkurugenzi wa VIWOTA, Vivian Ugulumu, anasema wameanzisha kampeni hiyo, baada ya kugundua ilivyo hali ya ugumba nchini inaongezeka, huku watoto wa umri miaka 10 hadi 13, wanazidi kutumia vinavyoachangia, kama dawa za uzazi wa mpango katika umri mdogo.

Pia, kuna suala la kufanya mapenzi katika umri mdogo, wanabakwa, wanalawitiwa, watoto wananyonyeshwa sehemu za siri, kunachangia watoto wadogo kupata magongwa ya zinaa katika umri mdogo.

Hadi sasa, zaidi ya wanafunzi 10,000 kutoka shule za msingi na sekondari katika mkoa wa Tanga na Dar es Salaam, wamepata mafunzo kuhusu ugumba na mengineyo.

Wanafunzi walionufaika na mafunzo hayo, ni pamoja na Shule ya Sekondari Usagara, Tanga na Dar e s Salaam, siko shule za msingi Barracks, Mivinjeni, Taifa, Salvation Army, huku sekondari ni za Lumo na Mbande.

"Wakati wa mafunzo, watoto wanafundishwa kujitambua, kusoma kwa bidii, kuacha tabia mbaya, matumizi mabaya ya dawa za kulevya katika umri mdogo, masuala ya ugumba, kutoa mimba katika umri mdogo, mahusiano katika umri mdogo, madhara ya kulawitiana, kusagana, utoaji wa mimba katika umri mdogo na madhara ya magonjwa ya zinaa katika umri mdogo," anasema.

Pia anataja kingine ni suala la kufundishwa elimu ya ujasiriamali, kujiamini, ukatili na unyanyasaji kijinsia, ili mtu anapopatwa na ukatili, aweze kusema masuala ya sheria, ili wajue jinsi ya kudai haki zao, hasa mzazi mmoja au wote wakifariki.

Ni mafunzo yanayotolewa vilevile kwenye jamii, kwa njia ya radio, televisheni na midahalo shuleni, hatua inayotolewa hali kadhalika kwenye likizo kwa watoto umri kuanzia miaka 5 hadi 15 waonafundishwa kujua aina ya ukatili wa kijinsia unaoweza kuwasababisha ugumba ukubwani.

Hapo kunatajwa matendo kama kunyonyeshwa sehemu za siri za kiume au kike, Ugulumu anafafanua: "Kutokana na mafunzo haya, hivi sasa baadhi ya watu wameanza kujitokeza kuripoti kesi, watu wanafanya biashara tofauti na miaka ya nyuma, wana amani, wagumba wengi wamejitokeza kusema..."

**KAMPENI ILIVYO**

Inatajwa lengo kuu ni kulinda kizazi cha sasa na kijacho, kuondoa unyanyapaa kwa wenye ugumba, kusaidia jamii na kutambua nafsi ya mgumba, huku ikisaidiwa serikali kulinda kizazi cha sasa na kijacho, kupunguza ugumba unaoweza kudhuru kizazi hicho, huku tiba yake ikipatikana.

Ofisa huyo anasema, kumeshuhudiwa katika zama zilizopo, watoto wadogo wanapitia changamoto nyingi za ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwa makusudi, ambao ni chanzo cha ugumba.

NINI KIFANYIKE?

Dhana pana inaelezwa ni kwa watu wote kupewa elimu kuhusu ugumba, ikiaminika ikitolewa vizuri kwa umma, ni rahisi kwa changamoto za ugumba kupata majibu sahihi.

Ni mtazamo wa kitaalamu unaooana na kuwataka wanaume wasiwe wagumu au wabishi kwenda hospitalini kupima afya zao katika eneo hilo, takwimu zikitajwa asilimia 80 ya wanaume hawaendi hospitali kutafuta matibabu, wakiamini wako sahihi.

"Mwanaume atajua kuwa yeye ni mgumba baada ya kwenda hospitali kupata vipimo na siyo mtu binafsi," anatamka Ugulumu, huku rai ikiitamkia serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama.

Ni suala linaloweka mvuto kwa umma, kufanya uchunguzi wa eneo hilo, huku ikwatambua na kuwathamini wagumba, wapate haki zao kama makundi mengine ya kijamii.

Uwiano wa kitakwimu unataja miaka ya nyuma, hali ya ugumba haikuwa juu kama ilivyo sasa, sababu inayotajwa ni watoto na vijana hawakutumia dawa za kizazi kuzuia mimba na kuongeza nguvu za kiume, kama ilivyo sasa.

**CHANGAMOTO ZA UGUMBA**

Kunatajwa ni kuwapo hali ya gumba katika jamii inazaa, athari zingine kama vile kuibuka matukio ya ama ukatili wa kijinsia kwenye jamii au usioendana na mtindo wa maisha.

Hapo kunatajwa matukio kama ya baadhi ya kinamama kuweka mimba za uongo, pia kunyimwa mirathi kwenye ndoa inapovunjika au penye kifo cha mzazi mwenza.

Inatajwa matukio ya mgumba anapofanya biashara katika jamii, anasimangwa, matukio hasa kwa vijijini wanakatishwa tamaa.

"Hawajui kuwa hata kama huna mtoto lazima ufanye kazi, utimize wajibu kama binadamu, bila ya kujali una watoto au huna, watoto kwa sababu jamii nzima inakutegemea. Una mama, baba, wadogo zako, watoto wa ndugu wote wanaweza kukutegemea, kwa sababu siyo familia zote zina uwezo," anasema.

**ALIYEASISI CHAMA**

Mwenyekiti na Mwanzilishi wa Chama cha Wagumba Tanzania, Shamila Makwenjula, anasema wanatafuta mfadhili atakayesaidia wanachama kupata vipimo vya afya, kujua kama wana tatizo. Hadi sasa wako 469 kutoka mikoa ya; Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Morogoro, Mara, Kagera, Tabora na Singida.

Mbali na hilo, chama kinahitaji vitendea kazi kama vile usafiri ili kufikia watu wengi zaidi na sasa hivi wana mkakati wa kutoa elimu nchi nzima ili jamii imtambue mgumba na hali yake na apate haki zake ndoa inapofika ukomo.

Shamila anafafanua: "Tumeamua kuja na mkakati huu baada ya kufanya utafiti katika mikoa yote kuhusu ukatili na unyanyapaa wanaofanyiwa wagumba mwaka 2020-2022, tukagundua kuwa wanawake wengi ambao ni wagumba wanamepata vipigo vilivyowapelekea kupata ulemavu wa kudumu, wamevunjwa miguu, mbavu, mikono, wengine wanabebeshwa mbwa kama mtoto na wengi wamekufa."

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Kassimu Pazzi, anasema, wameandika barua kwa Tume ya Haki za Binadamu, kutaka marekebisho ya kisheria katika eneo hilo la kijamii. Vilevile wanaandaa barua kama hiyo, kupata utambulisho wa serikali mikoani, ili wanapoanza kutoa elimu kwa jamii, kuhusu haki za wagumba.

MAZINGIRA

# Miaka 42 ya magugu maji Ziwa Victoria, vita vya kuyatokomeza

**Na Anthony Gervas, MWANZA**



Kikundi cha uwopoaji magugu maji Ziwa Victoria, wakiendelea na kazi yao. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

GUGU maji ni mmea ulioanza kuonekana Ziwa Victoria mwaka 1980. Hapo ndipo serikali ikapata wazo la kuanza kuukabili.

Ni kwa kipindi cha miaka 17, ndipo serikali za nchi tatu za Afrika Mashariki kunakofikiwa na Ziwa Victoria, ikiwamo, Kenya na Uganda, zikakaa na kuamua uanzishaji mradi.

Hiyo ikafanyika kwa kila nchi ikitekeleza kivyake kudhibiti usisambae ziwani humo. Hiyo ilikuwa mwaka 1997, pale Jumuiya ya Afrika Mashariki iliporejea, baada ya kuvunjika miaka 20 kabla, yaani mwaka 1977.

Ni baada ya mmea huo kuanza kustawi ziwani, ukasambaa kwa kasi majini na kusababisha wavuvi kushindwa kuvua samaki, meli, vivuko na boti kukwama kutia nanga kwenye mialo kwa ajili ya kushusha na kupakia abiria, pia mizigo.

Yanatajwa madhara ya magugu hayo yanageuka maficho ya wanyama wakali baada ya kuzaliana kwa kasi, wakiwamo mamba na viboko wanaovamia wavuvi safarini, madhara na vifo vikashuhudiwa.

**MAMLAKA VITANI**

Meneja wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) Kanda ya Ziwa, Martin Katua, anasema magugu maji huzaliana kwa njia mbili; kuota, pia mbegu zake.

"Magugu maji ni mmea wenye uwezo wa kuzaa mbegu kuanzia milioni tatu hadi milioni 10 na kukaa zaidi ya miaka 50, zikiwa na uwezo wa kuota," anaeleza Katua.

Anasema baada ya kuanzishwa mradi wa Hifadhi ya Mazingira (LVEMP) mwaka 1997 ulioisha muda wake mwaka 2018, wakati huo ukubwa wa eneo la magugu maji ilikuwa hekta 2,000.

Inatamkwa juhudi zilizofanyika ni kuanzisha vituo 17 vya uzalishaji wadudu aina ya Mbawakavu, kuwatumia kudhibiti magugu maji hayo.

Njia nyingine Katua anataja ni kutokomeza magugu maji kwa kutumia nguo maalumu, boti, reki na kamba.

Vilevile anafafanua hatua ya mafanikio hata yakapungua kusambaa kufikia ukubwa hekta hekta 400 mwaka 2005.

Anasema hadi kufikia mwaka 2010 magugu maji yaliongezeka hadi kufikia eneo lenye ukubwa wa hekta 731, lakini udhibiti ukaendelea kufanyika kupitia msaada wa LVEMP II kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya na jamii.

Ni usimamizi anaoutaja ulifanyika kupitia halmashauri za vijiji, zikisimamia Usafi wa Mialo na Udhibiti wa Uvuvi Haramu (BMU) na hadi kufikia mwaka 2017, magugu maji yalipungua kufikia hekta 103.

Ofisa Kilimo Mkuu Msaidizi Afya ya Mimea na ViatilifuTanzania (TPHPA) Kanda ya Ziwa, Enrisha Mbwambo, anasema kuna vikundi 39 vya wananchi vya uopoaji magugu maji hayo na kukabidhiwa miradi midogo ya uzalishaji mali.

Mbwambo anasema, lengo ni kuwanufaisha kiuchumi wananchi hao, baada ya kupewa mafunzo wakifuga samaki katika mialo ya Bagole, Nyahiti, Ilalambogo na Mbalika Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza.

Anaeleza kuna vikundi vingine vilipatiwa mradi wa ufugaji nyuki wa Nyakalilo wilayani Sengerema, kuanzisha masoko ya Kisolya na Mugara, ufugaji wa kuku na ukaushaji wa dagaa katika Wilaya ya Bunda mkoani Mara.

Mbwambo anasema, kikundi cha Sweya mkoani Mwanza na Kagera, kikundi cha Suguti, vilikabidhiwa mradi wa mitumbwi ya kusafirisha abiria na wilaya nyingine za mikoa hiyo kila moja, ilikuwa na mradi wake iliyochagua.

Anasema, mkakati wa mamlaka hiyo ni kuhakikisha inaendelea kutoa huduma bora katika kudhibiti visumbufu vya mmea ndani ya Ziwa Victoria, udhibiti wa ndege aina ya kweleakwelea na nzige kwa Kanda ya Ziwa.

Vingine anataja ni wadudu viwavijeshi naudhibiti wa magonjwa ya mlipuko kutoka nje ya nchi.

Anataja mafanikio ya mamlaka yao kwa mwaka jana, wamedhibiti viwavijeshi kushambulia mazao ya mpunga, pamba, mahindi, maharage na mihogo na kweleakwelea mlipuko wa magonjwa .

Anasema kwa kuwa TPHPA ni mpya, huduma zake bado zinasuasua na fedha za kutekeleza miradi na vyanzo vya mapato, ni kizungurumkuti.

**MADHARA NA CHANGAMOTO**

Mbwambo anataja madhara ya mmea huo inaharibu na kuathiri mazalia ya samaki, kuzuia vyombo vya usafiri, kuziba mitambo, mabomba ya kuvuta maji, kuchafua hewa safi ya maji na kujaza udongo ziwani.

Inatajwa, juhudi za kudhibiti magugu maji zinakabiliwa na magumu, ikiwamo shughuli za kibinadamu zinazoendelea kando ya ziwa, wakitiririshia maji kuongeza uchafu wa mbolea inayochochea kuzaliana mmea huo.

Hiyo inunganishwa na elimu duni kwa wananchi kwa kutumia magugu maji hayo kama mbolea shambani, kwa wakulima wa kando ya ziwa, maua yake yakifanywa malisho ya mifugo.

Inafafanuliwa, hadi kufikia 2017 magugu maji yalipungua hadi kufikia eneo la ukubwa wa hekta 103 kutoka zaidi ya hekta 400 mwaka 2005 kama inavyotajwa.

Vilevile, hadi sasa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania, inatarajia kuanzia mwezi ujao (Novemba) kuchukua hatua zingine kuendelea kudhibiti magugu maji hayo.

Inafafanuliwa kwamba katika mradi uliopita, jamii ilinufaika kwa kipato cha kufanya kazi za uopoaji magugu maji, kupitia vikundi vya halmashauri za wilaya kwa kuanzisha miradi ya masoko na vyoo vya kulipia.

# UNDANI WAKE MRADI MAJI VICTORIA ALIYOUZINDUA RAIS SAMIA SINGIDA

**Inatoka Uk. 11**

maji, wanaharibu vyanzo vya maji. Wawekezaji wakubwa, waache kuiba maji, bali wachimbe visima vya maji na siyo kutuibia maji.

"Wale ambao wanachepusha maji waache, wote waliofanya hivyo wabomoe hivyo vizuizi walivyoweka kwani kila mwananchi anahitaji maji. Wizara ya Maji na Bonde, mlishughulikie hili," anatamka Makamu wa Rais.

"Ni ni ajabu tena wanaoiba maji ni wawekezaji wakubwa na mnawatoza faini ndogo, nawaonya muache! Vyombo vya usalama, vifuatilie kubaini wezi wa maji, hao wawekezaji wanaoiba maji wachimbe visima vya maji, wavune maji," anasema Dk. Mpango.

"Nimefurahi kusikia watumishi idara ya maji yamebadilika, lakini masikio yangu kwa wananchi bado kuna malalamiko ya wananchi kubambikiwa bili za maji. Na hapa mbadilike, wananchi wanasema wakati mwingine wasoma mita hawasomi mita, wanakadiria, nataka wabadilike, watoe bili kadiri wananchi walivyotumia," ananena Dk. Mpango, mtaaluma wa uchumi.

Vilevile, anawasihi watumishi wa wizara yake na mamlaka za maji ziliko, ziendelee kutunza miundombinu hiyo ya maji na mazingira ili miradi uwe endelevu na kuwahudumia wananchi kwa muda mrefu.

"Napenda kuwakumbusha wananchi kushirikiana kutunza miundombinu ya maji na kutunza mazingira kwa kupanda miti na maua kwenye maeneo yetu, ili kunusuru nchi yetu iliyoathiriwa na ukataji miti bila ya kupanda mipya.

"Nataka miti mingi zaidi ipandwe hapa tulipo. Ni lazima turejeshe uoto wa asili, hili suala la kuhifadhi mazingira kwenye vyanzo vya maji ni lazima, ni lazima tulinde vyanzo vya maji. Uharibifu wa vyanzo vya maji ni hatari... msione Ziwa Victoria ni kubwa, linaweza kukauka, tukikosa maji tutakufa, tusichukulie kawaida hili," anafafanua Dk. Mpango.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, katika kipindi cha serikali ya awamu ya tano, kati ya mwaka 2015 hadi 2019, kuna jumla ya miradi ya maji iliyotekelezwa na serikali iko 1,423; vijijini ilikuwa 1,268 na mijini 155.



# Vijiji 4,072 kufikishiwa huduma ya umeme

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) kupitia mradi wa awamu ya tatu mzunguko wa pili imejiwekea lengo ifikapo Juni 2024 vijiji 4,072 vitakuwa vimefikiwa na huduma ya umeme.

Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Hassan Saidy, aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa mradi wa umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili unaovihusisha vijiji 120 vya Wilaya ya Iramba mkoani Singida ambao ulifanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema utekelezaji wa mradi huo kwa vijiji vilivyobaki utagharimu Sh.trilioni 1.6 na kwamba mpaka sasa vijiji 11,000 vina umeme na vijiji 1,300 vilivyobaki vitafikiwa ifikapo Juni 2024.

**Asilimia 90 ya kazi yote imekamilika na tunatarajia ifikapo Juni mwakani Mkoa wa Singida wote utakuwa unawaka umeme.**

Saidy alisema REA tangu ilipoanzishwa mwaka 2007 kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) umesaidia kuongeza hali ya upatikanaji umeme vijijini kwa upande wa Tanzania Bara kutoka asilimia 5 mwaka 2007 hadi 70 mwaka 2020 tathmini ya mwisho ilipofanyika.

Aidha, alisema kupitia miradi mbalimbali ya umeme vijijini, Serikali kupitia REA kati ya vitongoji 64,760 vilivyopo nchini, vitongoji 28,659 sawa na asilimia 44 vishafikiwa na huduma ya umeme.

Alisema serikali inaendelea na mipango ya kuongeza mafungu katika Mfuko wa Nishati Vijijini ili kuongeza kasi ya kufikisha umeme katika vitongoji 36,101 vilivyobaki kupitia mpango wa kufikisha umeme vitongoji vyote.

Aliongeza kuwa mbali na shughuli za uchumi na huduma za jamii, umeme vijijini umesaidia kuboresha ulinzi, kuhifadhi mazingira, kuimarisha usawa wa kijinsia pamoja na kuchangia azma ya serikali katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) ambapo upatikanaji wa nishati bora utasaidia kufikia malengo 13 kati ya malengo 17.

"Hivi tunavyoongea serikali yako inatekeleza miradi mikubwa saba ya kupeleka umeme maeneo ya vijijini kupitia kandarasi 112 ambayo kwa ujumla wake itapeleka umeme katika vijiji na vitongoji takribani 11,000," alisema.

Saidy alisema mradi huu wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili ndio unaenda kuhitimisha safari ya kufikisha miundombinu ya umeme katika vijiji vyote 12,318 Tanzania Bara kama ambavyo imeelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 kuwa ifikapo mwaka 2025 vijiji vyote viwe vimefikiwa na huduma za umeme.

Rais Samia akizungumza na wananchi baada ya kuzindua mradi huo, alisema Wilaya ya Iramba ni sehemu ya mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa pili ambao unalenga kufikia vijiji 178 vilivyopo katika wilaya za Singida vijijini, Mkalama, Manyoni, Ikungi na Iramba.

"Asilimia 90 ya kazi yote imekamilika na tunatarajia ifikapo Juni mwakani Mkoa wa Singida wote utakuwa unawaka umeme," alisema.

Rais Samia alisema serikali inaendelea kuchukua hatua za muda mfupi na mrefu za kuimarisha gridi ya taifa ili kuondokana na kero ya umeme kukatika mara kwa mara.

## Bunge lashauri kupanuliwa fursa za ajira wanaoishi ughaibuni

**Na Augusta Njoji,** Dodoma

KAMATI ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii imeishauri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kupitia kitengo cha huduma za ajira kupanua wigo wa fursa za ajira kwa Watanzania nje ya nchi.

Akizungumza jana katika kikao cha kamati hiyo cha kupokea na kujadili utendaji kazi wa kitengo hicho, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Fatuma Toufiq, alisema pamoja na juhudi za serikali kufungua fursa za ajira kuna umuhimu wa kuhamasisha Watanzania kuchangamkia fursa za ajira nje ya nchi.

Pia, alishauri kufanyika kampeni maalum ya kukutana na wakala binafsi wa ajira ili kuwajengea uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliahidi kufanyia kazi maoni ya kamati, huku akimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa hatua ambazo amezichukua za kukuza uwekezaji nchini na kufungua fursa za ajira kwa Watanzania.

Kadhalika, Naibu Waziri wa ofisi hiyo, Patrobas Katambi, aliwahimiza Watanzania wanaotaka kufanya kazi nje ya nchi kufuata utaratibu unaotambulika na serikali ili iwe rahisi kusaidiwa wanapopata changamoto.

Awali, Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema kitengo hicho kimetokana na kufutwa kwa Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA) na majukumu yake kuunganishwa chini ya Idara ya Ajira na Ukuzaji Ujuzi.

Akitoa taarifa kwa kamati, Mkurugenzi wa kitengo hicho, Joseph Nganga, alisema miongoni mwa majukumu ya kitengo ni kuwajengea uwezo wahitimu kushindana kwenye soko la ajira, kujenga mtazamo chanya kuhusu kazi na kukuza maadili yanayohitajika na waajiri.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kulia), akizungumza wakati akifungua semina ya kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya mkoa huo jana. Wa (pili kulia) ni Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa (Viwanda, Biashara na Uwekezaji), Mwajabu Nyamkomora. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## H/shauri kumshika mkono mwanamke wa kijijini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imesema itaendelea kutatua kero zinazomkabili mwanamke wa kijijini katika uzalishaji wa chakula na kusimamia lishe ya familia.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Charity Sichona, aliyasema hayo kuhusu maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Duniani anayeishi kijijini ambayo yatafanyika katika Kata ya Chihanga jijini Dodoma.

Sichona alisema Jiji la Dodoma linaadhimisha siku hiyo kwa lengo la kuendelea kutambua jitihada za mwanamke anayeishi kijijini ili kuzidi kumtia moyo katika shughuli zake za kila siku.

"Wanawake wanaoishi vijijini wanamchango mkubwa katika kuzalisha chakula na kuchangia uwepo wa chakula katika familia na nchi nzima, wanapaswa kuheshimiwa na kupewa ushirikiano," alisema Sichona.

Alifafanua kuwa serikali imeamua kutambua jitihada zao za kilimo, ufugaji na shughuli za kiuchumi ikiwamo kuwatia moyo ili waendelee kuzalisha wakati serikali ikiendelea kutatua kero zinazowakabili katika maeneo mbalimbali.

Sichona alisema kuwa, mwanamke wa kijijini anapowezeshwa kufanya shughuli zake bila vikwazo vya familia, halmashauri na taifa kwa ujumla litakuwa na uhakika wa chakula cha ziada.

Akizungumzia kuhusu baadhi ya programu zinazowezeshwa na serikali kwa wanawake alisema kuwa zipo kwa ajili ya kuwasaidia wanawake kukua kiuchumi ili waweze kupiga hatua katika shughuli zao za kila siku.

"Rais, amewezesha programu mbalimbali. Mfano kizazi cha usawa, hii inatambua jitihada za wanawake wanazofanya na wanapewa elimu juu ya uzalishaji, masuala ya kilimo, mifugo na kazi za mikono ili kuendeleza uchumi wao na kuleta usawa katika kumiliki mali na ardhi," alisema Sichona.

Naye Mkazi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Hadija Sued, alisema kuwa ni mara yake ya kwanza kusikia maadhimisho hayo ambapo alisema ni ya muhimu kwa sababu yatawahamasisha wanawake kuongeza juhudi katika shughuli zao za uzalishaji mali.

Kutokana na hilo alisema serikali imefanya vizuri kuanzisha maadhimisho ya mwanamke anayeishi kijijini ambayo yatasaidia kutoa mwamko kwa wanawake wa vijijini kufanya kazi kwa bidii ili kujiinua kiuchumi.





# Hospitali ya Kanda yabuni gari la kubeba wagonjwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, imebuni magari maalumu ya kubeba wagonjwa ndani ya hospitali hiyo ili kurahisisha kuwahamisha wagonjwa kutoka wodi moja kwenda nyingine.

Magari hayo yalizinduliwa juzi na kuanza kutumika ambapo inaelezwa kuwa yataongeza ufanisi kwenye utoaji wa huduma kwa wagonjwa ndani ya hospitali hiyo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa magari hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, alisema magari hayo yamebuniwa na wataalamu wa idara ya uhandisi ndani ya hospitali hiyo.

Alisema magari hayo yatakuwa yanatumika kubeba wagonjwa wasio na uwezo wa kutembea wanaokwenda kutibiwa hospitalini hapo.

Alisema ubunifu wa gari hilo maalumu utapunguza tatizo la watoa huduma ambao hapo awali walikuwa wakitumia viti mwendo

**Magari hayo yatakuwa yanatumika kubeba wagonjwa wasio na uwezo wa kutembea wanaokwenda kutibiwa hospitalini hapo.**

pamoja na vitanda vya magurudumu kupeleka wagonjwa maeneo mbalimbali ya kutolea huduma hospitani.

Alisema pia yatasaidia kuongeza tija kwenye utoaji wa huduma kwa wagonjwa ndani ya hospitali hiyo.

"Gari hili linaenda kuchukua nafasi ya vile viti mwendo na vitanda vya magurudumu, hivyo kusaidia kutokuwa na kazi ya kutumia nguvu wakati wa kuwabeba wagonjwa na hivyo kuwasababishia wengi shida za migongo," alisema Dk. Mbwanji.

Aliishukuru serikali kupitia Wizara Afya kwa mchango wa kuunga mkono huduma mbalimbali za afya zinazotolewa hospitalini hapo pamoja na ubunifu unaofanywa na wataalamu wa sekta ya afya katika kuboresha huduma za afya nchini.

Dk. Mbwanji alipongeza idara ya uhandisi hospitalini hapo kwa bunifu mbalimbali zinazofanywa ikiwamo za mfumo wa kumpa taarifa mtoa huduma wakati mgonjwa anapohitaji msaada pamoja na mfumo wa kurekebisha hali joto katika chumba cha watoto wachanga.

Mmoja wa wataalamu kutoka katika idara ya uhandisi ya hospitali hiyo, Fredrick Ndondole, alisema wazo hilo lilitoka kwa uongozi wa hospitali na utekelezaji ukafanywa na kitengo chao cha uhandisi ambacho kilitekeleza kwa kufuata mawazo ya kitaalamu.

Alisema gari hilo ni rafiki kulingana na mazingira ya hospitali hiyo kutokana na kuwekwa vizuri ikiwamo barabara zinazounganisha wodi moja na nyingine.

"Tulipokea wazo hili kutoka kwa mkurugenzi wa hospitali kutokana na changamoto iliyokuwa ikiwapata watumishi kutokana na kusukuma wagonjwa kwa mikono kwa kutumia viti mwendo na vitanda vya magurudumu," alisema Ndondole.

Baadhi ya wauguzi wa hospitali hiyo walisema magari hayo yatawasaidia kupunguza kazi ya kuwasukuma wagonjwa kwenye viti mwendo na vitanda na kwamba teknolojia hiyo inaendana na mabadiliko ya dunia ya sasa.

Mmoja wa wauguzi hao, Alta Mpogole alishukuru uongozi wa hospitalini hiyo na kusema uwepo wa gari hilo maalumu la kubeba wagonjwa litakuwa msaada kwa kuwa hapo awali walikuwa wakitumia viti mwendo pamoja na vitanda vya magurudumu.



Mkuu wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Jafar Haniu (kulia), akimiminiwa maji ya mgomba pori kwa ajili ya kunywa na mmoja wa maofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS), alioambatana nao wakati akikagua uharibifu wa mazingira ndani ya msitu wa Uporoto ambao ni sehemu ya Hifadhi ya Msitu Asilia wa Mlima Rungwe, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Miezi mitatu migogoro 30 ya ardhi yapokelewa Makete

**Na Elizabeth John,** MAKETE

SHIRIKA la Msaada wa Kisheria (MAPAO) lililopo wilayani Makete Mkoa wa Njombe, limesema kwa kipindi cha Julai hadi Septemba limepokea mashauri 93.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Mchungaji Denis Sinene, aliyataja mashauri hayo kuwa ni migogoro ya ardhi (30), ndoa (27), matunzo ya watoto (14), madai (10), ukatili wa kijinsia sita pamoja na unyanyasaji sita. Mchungaji Sinene alisema bado mashauri yanayohusu ukatili kwa wanandoa, watoto na kutelekeza yanaripotiwa kwa wingi hali inayoonesha jamii inauelewa sasa kuhusu masuala ya haki za kibinadamu.

Sinene alitoa wito kwa wananchi kusuluhisha migogoro yao kabla ya kukimbilia mahakamani kwani baadhi yao hupoteza muda wao kwa kushindwa kutambua sheria na utaratibu wa kesi.

Alisema ni vyema kutumia njia ya kusuluhisha na ikishindikana ndipo wapeleke mashauri yao katika ngazi za Mahakama ili kujenga jamii yenye ustawi na salama.

Pia alisema bado elimu inahitajika kuendelea kutolewa kwa jamii haswa wanandoa kwani baadhi yao wamekuwa wakifanya vitendo visivyo sitahili kwa wenza wao ikiwemo kunyimwa unyumba, kupigwa na kutelekezwa bila kuhudumiwa katika ndoa.

**Bado elimu inahitajika kuendelea kutolewa haswa wanandoa kwani baadhi yao wamekuwa wakifanya vitendo visivyo sitahili kwa wenza wao.**

# Waomba kushirikishwa katika vyombo vya uamuzi

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAKULIMA mkoani Mbeya wameiomba serikali iwashilikishe kwenye vyombo vya uamuzi kuanzia ngazi ya kijiji mpaka taifa ili kupunguza kero zinazowakabili likiwamo suala la upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati.

Ombi hilo lilitolewa juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani ambayo kimkoa yalifanyika wilayani Kyela na kushirikisha wakulima na viongozi mbalimbali wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima (MVIWATA).

Mwenyekiti wa MVIWATA Mkoa wa Mbeya, Sylivester Salawa, alisema wakulima wadogo wanatakiwa kushirikishwa kwenye vikao mbalimbali vya uamuzi ili wapate huduma ambazo wanastahili kutoka serikalini.

Alisema vikao vinatakiwa vianzie kwenye ngazi ya vijiji mpaka taifa kwa maelezo kuwa kundi hio limekuwa likisahaulika mara kwa mara na hivyo kupatiwa huduma ambazo wakati mwingine zinakuwa siyo shirikishi.

"Tunatakiwa tuwe tunashiriki kwenye vikao vya uamuzi, tunatakiwa tuwe na viongozi kuanzia ngazi ya vijiji, watakuwa wanatuwakilisha kwenye vikao vya wilaya mpaka mkoani, hii itatusaidia kupunguza malalamiko," alisema Salawa.

Alisema yamekuwa yakiibuka malalamiko mbalimbali ya wakulima kuhusu mbolea na pembejeo zingine na kwamba matatizo hayo huwa yanasababishwa na kutoshirikishwa.

Katibu wa MVIWATA Mkoa wa Mbeya, Benjamin Mbilinyi, alisema moja kati ya kero zinazowakabili wakulima wadogo ni migogoro ya ardhi baina yao na makundi mengine yanayotumia ardhi hiyo wakiwamo wahifadhi.

Alisema baadhi ya maeneo yamekuwa yakichukuliwa na serikali na kufanywa kuwa misitu ya hifadhi hali ambayo inasababisha maeneo ya kilimo kupungua na hivyo uzalishaji kupungua.

"Lakini baadhi ya maeneo yanachukuliwa na wawekezaji wakubwa na wengine hawayaendelezi, kwahiyo tunaiomba serikali iwe inatushirikisha kwenye uamuzi," alisema Mbilinyi.

Mmoja wa wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa MVIWATA, Mariam Wakuganda, alisema wakulima wadogo ndio msingi wa uhakika wa chakula nchini na hivyo ni lazima walindwe kwenye maeneo mbalimbali.



# Mfumo wa elimu Z'bar kufumuliwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar inatarajia kufanya mabadiliko ya mfumo wa elimu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri wa wizara hiyo, Lela Muhammed Mussa, alisema ili kubadilisha kwa mfumo huo mpya lazima Wizara ya Elimu ibadilishe sera yake ya mwaka 2006 pamoja na Sheria ya Elimu ya Mwaka 1982.

Alisema mabadiliko hayo kwa upande wa Zanzibar ni makubwa, hayajawahi kutokea hivyo lazima kuna baadhi ya vitu vitabadilika katika mitaala ya elimu.

**Hivi sasa vijana wengi wanaelimu ya juu, kiwango cha uzamili lakini katika fani alizosomea hana ujuzi wowote kutokana na kukosa msingi mzuri.**

Waziri huyo alisema katika mabadiliko hayo elimu ya mafunzo ya amali (ufundi) itakuwa ni suala la lazima kwa mwanafunzi wa Zanzibar ili wanapomaliza masomo yao wawe na uwezo wa kujiajiri.

Alisema lengo la serikali kupitia Wizara ya Elimu ni kumtayarisha kijana kusima ma katika masomo ya fani ili anapomaliza masomo yake awe na uwezo wa kujua kazi za ufundi kwa kivitendo.

"Hivi sasa vijana wengi wanaelimu ya juu, kiwango cha uzamili lakini katika fani alizosomea hana ujuzi wowote kutokana na kukosa msingi mzuri," alisema.

Alisema licha ya mabadiliko hayo lakini yataanza kwa wale wanafunzi wa darasa la kwanza kwa mwaka wa 2023 lakini waliokuwapo katika elimu hivi sasa wao wataendelea na mfumo uliyopo.

Alisema katika kuhakikisha kuwa mabadiliko hayo yanaleta tija serikali kupitia Wizara Elimu inatarajia kurudisha Chuo cha Uwalimu ili walimu wakasomeshwe mbinu bora za kufundishia.

Alisema jambo hilo siyo geni na miaka iliyopita kulikuwapo kwa chuo kama hicho na walimu walikuwa wanafundishwa juu ya mbinu imara za kuwafundishia wanafunzi wa shuleni.

Pia alisema wizara imejipanga juu ya jambo hilo kubwa ikiwamo kuanzisha Tume ya Utumishi na Maadili ya Walimu ambayo itaimarisha usimamizi na upangaji wa nguvu kazi ya walimu bila ya kuingiliana kimajukumu na vyama vya wafanyakazi.

Alisema hatua hiyo inaenda kuimarisha kada ya walimu kuwa katika misingi imara katika mambo yanayowahusu katika kazi yao hiyo ya uwalimu.

## Waziri ahimiza wananchi kulinda vyanzo vya maji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduwara, amewataka wananchi kulinda vyanzo vya majisafi na salama kwa ajili ya mikakati ya kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji mashambani.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi ikiwamo wakulima katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Chakula huko Chamanangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema mikakati ya serikali ni kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji kwa ajili ya kujitosheleza na chakula na kuondokana na tatizo la uagiziaji chakula nje ya nchi.

Aidha, alisema uzalishaji wa majisafi na salama umefikia asilimia 67 katika mwaka 2023 kutoka asilimia 56 mwaka 2022 ambapo lengo ni kufikia asilimia 76.

Alisema katika fedha za miradi ya Uviko- 19 kwa asilimia 67 serikali imeelekeza fedha hizo katika upatikanaji majisafi na salama ikiwamo ujenzi wa visima na matangi ya kuhifadhi maji.

Kaduara alisema serikali pia imefanya mambo makubwa ikiwamo kuongeza bajeti ya kilimo hadi kufikia asilimia 84 kutoka bajeti ya Sh.bilioni 53.590 hadi kufikia Sh.bilioni 98.716 katika mwaka 2023.

Alisema juhudi hizo hazitafanikiwa kama wananchi wataendelea kuharibu vyanzo vya majisafi ikiwamo ujenzi wa holela katika maeneo ya mashamba ya kilimo.

''Hiyo ni sehemu ya mikakati ya kukuza sekta ya kilimo pamoja na umwagiliaji mashambani katika kilimo cha mpunga kuona kwamba tunajitosheleza kwa chakula,'' alisema.

Aidha, alisema mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kujitosheleza kwa chakula ikiwamo cha mpunga na kupunguza uagiziaji nje ya nchi.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa barabara kutoka mjini Zanzibar kwenda Mkoa wa Kusini Unguja kwa kiwango cha lami katika eneo la Jumbi, hivi karibuni. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mama Mwinyi aipongeza UWT kwa kuwajali wanawake, vijana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MLEZI wa Jumuiya ya CCM ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi ameipongeza jumuiya hiyo kwa kuwa na viongozi imara wenye dira ya maendeleo endelevu na mioyo ya kujituma, kuwapambania wanawake na vijana.



Aliyasema hayo wakati akizungumza na uongozi wa UWT ukiongozwa na Katibu Mkuu wake, Jokate Mwegelo na ujumbe wali ofika Ikulu ya Migombani, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Mama Mariam Mwinyi ambaye ni Msarifu na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), alieleza uongozi huo kuhusu taasisi ya ZMBF inavyounga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia sera yake ya uchumi wa buluu.

Alisema taasisi ya ZMBF imewawezesha kiuchumi wanawake na vijana hasa wakulima wa mwani baada ya kuwaweka pamoja kinamama wa Unguja na Pemba kwa lengo la kuwapa mikopo nafuu ili kuendeleza zao hilo.

Alisema kilimo cha mwani Zanzibar kinachangia asilimia tatu katika Pato la Taifa baada ya utalii unaochangia asilimia 30.

Mama Mariam alisema mbali na fursa nyingi zinazotokana na mwani ikiwamo kutumika kama, chakula, dawa, vipodozi, virutubisho vya mwili na kuongeza lishe mwilini pia zao hilo linaimarisha afya za wajawazito.

Kadhalika, alimpongeza Katibu Mkuu Jokate Mwegelo kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo na kukipongeza CCM kwa kufanya uteuzi sahihi.

Naye Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania, Jokate Mwegelo, alisema UWT inabeba agenda zote zinzazowahusu wanawake bila kujali tofauti zao kisiasa, dini, ukabila, rangi wala kipato na uchumi wao.

Pia alipongeza mabadiliko ya maendeleo yanayofanywa na Rais Dk. Mwinyi kwa kipindi kifupi Zanzibar imekuwa na maendeleo makubwa na kusifu jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa kwenye suala zima la kuimarisha miundombinu ya barabara na mawasiliano.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

LUCKSON LAULIAN MAINGU anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya BOXER yenye usajili namba MC 452 CTE, CHASSIS NAMBA: MD2B15BX8LWG9 na ENGINE NAMBA: JVXWLG07168. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: NJB/TR/RB//2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

MONICA CHANGAMIKE anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 725 AZZ aina ya Toyota MARKII. Chassis No. GX1006135903. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: PHQ/DOD/DOD/5949/2023

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SINGIDA**
**LILILOPO SINGIDA**
**SHAURI LA MAOMBI YA ARDHI NA. 06 YA 2020**
**DERICK PACKIEL BARAKA……………….MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**FAISAL SEMBUA MFINANGA……………..MJIBU MAOMBI NA. 1**
**JUMA SHABANI JUMA……………………..MJIBU MAOMBI NA. 2**

**KWA: JUMA SHABANI JUMA – POPOTE WALIPO TANZANIA**

### KUITWA SHAURINI:

Kwa kuwa Mwombaji tajwa hapo juu ameleta maombi yake hapa Barazani ambayo maelekezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi, ambayo yanaweza kupatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria hapa Barazani tarehe 24/10/2023 saa 2:00 asubuhi siku ya kutajwa kwa shauri hilo. Unatakiwa kuhudhuria mwenyewe au muwakilishi wako anaetambuliwa kisheria siku na saa tajwa hapo juu.

ANGALIA: Kushindwa au kupuuza kufika tarehe na saa iliyotajwa hapo juu kesi itapangwa na kusikilizwa ikiwa na mleta maombi na mjibu maombi Na. 1 tu na uamuzi kutolewa bila ya wewe au mwakilishi wako kuwepo.

HATI hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya BARAZA hii leo tarehe 12 Mwezi wa October, Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA
SINGIDA.

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA WILAYA SONGWE**
**LILILOPO MBOZI**
**SHAURI NA.23/2023**
**KAWAWA M.SHANTIWA::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**1.ALMAS M.SHANTIWA::::::::::::MDAIWA**
**2.ALMAS M.SHANTIWA:::::::::::::MDAIWA**
**3.EDGA JIMSON::::::::::::::::::::::::MDAIWA**
**4.FRANK PISON::::::::::::::::::::::::MDAIWA**
**YAH:KUITWA SHAURINI**
**KWA:ALMAS M.SHANTIWA,ALMAS JIMSON,EDGA JIMSON,FRANK PISON**

Fahamu kwamba KAWAWA M.SHANTIWA amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kusikilizwa tarehe 19/10/2023 saa 2:30 asubuhi,mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.

Namriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la mnadani-Vwawa.

Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo hukumu itasomwa pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 21/09/2023.

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**21/10/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 129 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late**
**ASAN YOHANA MALUGU**
**of Mpunguzi within Dodoma City**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ALFERD ASSAN MALUGU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of 11,2023

Dated at Dodoma this 10 Day of 10, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NPAYAS REUBEN MOREMI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye umiliki wa jina la KELKEN INVESTMENT namba yake ya usajili ni T 975 BHJ. Chassis No. GX1100005686. Engine No. IG6838973. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: PHQ/DAR/KIN/24773/2023.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 76/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU PETER MAPINDA MAGUZU wa NKUHUNGU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA 1. SELESTINE PETER MAGUZU**
**2. RHODA PETER MAGUZU**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03 Mwezi 11Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 18 Mwezi 10 Mwaka 2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NDELEKWA YESAYA KAAYA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya MITSUBISHI PAJERO yenye usajili namba T 163 BSB , CHASSIS NAMBA: YHNV3601J000208 na ENGINE NAMBA: DH7851. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/4116/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHNSON JONATHAN MBASHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **LANDROVER DISCOVERY** yenye usajili namba **T 377 DZM**, Chassis No. **SALLAAA136A3833387**, Engine No. **0105276276DT.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/27416/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

S & Y WOOD PRODUCTS COMPANY LIMITED anatangaza kupotea kwa plate number na kadi ya gari aina ya PHOTON SEMI TALLER yenye namba za usajili T 841 DFS Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: PHQ/DOD/DOD/5907/2023; Taarifa ya Polisi: PHQ/DOD/DOD/5905/2023.

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA LESENI YA UCHIMBAJI MADINI

MWADAWA JOHN MSEMO ANATANGAZA KUPOTELEWA NA LESENI YA UCHIMBAJI MADINI YENYE NAMBA ZA USAJILI 002489 NZ TAARIFA HII IMETOLEWA KITUO CHA POLISI TAREHE 16 OKTOBER 2023 KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU. TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/4682/2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**USIMAMIZI WA MIRATHI Na……113/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU WORLD LEONARD MAKENGO WA KIHONDA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA SEMVUA LEONARD MAKENGO**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(20ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika Shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07 Mwezi 11 Mwaka 2023,kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo.

ZINGATIA:

Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa

Marehemu hakuacha Wosia

Imetolewa leo tarehe 13 mwezi 10 mwaka 2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ASIFIWE JOHANES KYANDOH** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA HARRIER yenye usajili namba : T 805 DDF, CHASSIS NAMBA: NOACU350001717 na ENGINE NAMBA: 2AZ1107728. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/4116/202**

***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

# Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




Wakazi wa Gaza wakilia baada ya Hospitali ya Al Shifa kushambuliwa jana. **PICHA: MTANDAO**

# Hamas, Israel walaumiana shambulio Hospitali Gaza

- **Israel yakanusha kuhusika**
- **Yanyooshea kidole kundi la Islamic Jihad**

**TEL AVIV, Israel**

PANDE mbili zinazohusika na mzozo wa Gaza, kundi la Hamas na Israel zimeendelea kulaumiana baada ya shambulio lililoilenga Hospitali ya Al-Ahli al-Arabi na kuwaua mamia ya Wapalestina katika ukanda wa Gaza.

Baada ya shambulio hilo lililotekelezwa jana maofisa wa Palestina wameilaumu Israel kuwa ilifanya shambulio la anga lililosababisha mlipuko mkubwa uliowaua mamia ya watu.

Walisema wanaamini kuwa Israel ilifanya shambulio hilo bila tahadhari katika hospitali hiyo iliyokuwa ikitumiwa kama hifadhi kwa mamia ya wakazi wa Gaza ambao hawana pa kuishi kutokana na mfululizo wa mashambulizi ya anga ya Israel.

Aidha, Israel ilikataa kuhusika na tukio hilo ikisema kundi lenye siasa kali za Kiislamu Islamic Jihad ndilo lilihusika kwa roketi zilizokosea njia na kuipiga hospitalini.

Baada ya mlipuko huo, madaktari katika mji wa Gaza waliripotiwa kukabiliwa na uhaba wa vifaa tiba na dawa huku wakilazimika kufanya upasuaji sakafuni ili kuwaokoa waathiriwa wa shambulizi hilo.

**WITO**

Kutokana na tukio hilo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, alitoa wito kwa pande mbili za mzozo huo kuweka chini silaha, huku akionya Israel kwa kile alichokiita adhabu ya jumla kwa watu wote wa Palestina.

Mkuu wa Sera za Kigeni wa Umoja wa Ulaya (EU), Josep Borell, alisema waliohusika na mashambulizi hayo wanapaswa kufichuliwa na kuwajibishwa.

Akizungumzia pia mlipuko huo, Mkuu wa Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa, Tedros Ghebreyesus, alisema hali katika Ukanda wa Gaza imefikia hatua ambayo inashindwa kudhibitiwa na kuwa pande zinazohusika katika mzozo huo hazina budi kusimamisha mapigano.

Ilibainishwa kuwa tangu Hamas ifanye mashambulizi Israel, Oktoba 7, mwaka huu takriban watu 1,300 waliuawa Israel na zaidi ya 3,000 wanakadiriwa kuuawa Palestina.

BIDEN ASITISHA ZIARA

Ilielezwa kuwa kutokana na mlipuko huo Rais wa Marekani, Joe Biden, ameahirisha ziara yake ya Jordan akiwa njiani kuelekea Israel.

Pia ilibainishwa kuwa kughairishwa kwa ziara hiyo kulitokana na serikali ya Jordan iliyotangaza kwamba mkutano wa kilele uliopangwa kufanyika jana kati yake na viongozi wenzake wa Jordan, Misri na Palestina umeahirishwa.

Uamuzi huo ulichukuliwa baada ya Rais Mahamoud Abass wa Palestina kuamua kuondoka Amann ambako alipanga kuhudhuria mkutano huo akiwa amekasirishwa na shambulio dhidi ya hospitali inayosimamiwa na kanisa la Baptist mjini Gaza, la Al-Ahli Arab.

Kila upande katika vita hivyo vya Ukingo wa Gaza unamlaumu mwengine kwa mlipuko huo mkubwa uliotikisa hospitali hiyo.

Kundi la wanamgambo wa Hamas, lilidai kwamba mamia ya watu waliouliwa walikuwa wamepata hifadhi hospitalini hapo, wakiwa ni familia, wagonjwa, watoto na wanawake. Huku maofisa wa Palestina wakisema zaidi ya watu 500 waliuliwa kutokana na shambulio hilo kubwa.

**ISRAEL YAKANUSHA**

Licha ya malalamiko hayo, Jeshi la Israel, (IDF) lilikanusha kuhusika na shambulio hilo, likidai kwamba lilifanywa na kundi la wanamgambo la Islamic Jihad ambalo lilifyetua roketi ambayo haikufanikiwa kufyatuka kwenda mbali na kuangukia kwenye hospitali hiyo.

Aidha, Kundi la Islamic Jihad, nalo lilitoa taarifa likikanusha pia kuhusika na shambulio hilo.

Wizara ya Ulinzi ya Pentagon ilitoa taarifa ikisema kwamba haijapata bado uthibitisho juu ya nani alihusika na shambulio hilo lililotokea angani dhidi ya Hospitali ya Al-Ahli Arab.

Hayo yakitokea White House ilitoa taarifa karibu na wakati ule ule ambao Rais Joe Biden anachukua ndege kuelekea Mashariki ya Kati, ikieleza kwamba Rais amesikitishwa na kukasirishwa sana baada ya kupata habari za shambulio hilo.

Taarifa ilieleza kwamba rais mara moja alituma rambi rambi zake kwa watu waliouliwa ambao hawakuwa na makosa na kuwatakia waliojeruhiwa afweni ya haraka.

**MAANDAMANO YAZUKA**

Baada ya shambulio hilo, ilielezwa kuwa maelfu ya watu waliingia mitaani katika nchi za Kiarabu kushutumu kitendo hicho cha mashambulizi mengi ya anga kwenye Ukanda wa Gaza.

Ilielezwa kuwa Wapalestina walikusanyika katika miji mikubwa kama Hebroni, Ramallah, Nablus, Tulkarem, Bethlehem, Tubas na Jenin. Aidha, mikutano mingi iligeuka kuwa makabiliano makali na polisi wa Palestina.

Pia ilibainishwa kuwa katika Jiji la Jenin, ilikuwa mshtuko wakati wakazi walipopata taarifa kuhusu hospitali hiyo kushambuliwa, jambo lililoibuwa misikiti ya jiji hilo na kuitisha mkusanyiko mkubwa.

"Watu wa Jenin hawakubali dhuluma au maumivu ya watu wa Gaza. Maandamano haya yameandaliwa kupinga uhalifu wa kivita unaofanywa na Israel. Lakini hapa Jenin Mamlaka ya Palestina, wasaliti hawa, wahaini hawa, walitaka kuvunja maandamano yetu.

"Kutokana na upinzani wetu, tuliweza kupambana. Na Mungu atuepushe na Abu Mazen na mamlaka yake," alisema mmoja wa wakaazi wa Jenin.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa mitaani, waandamanaji walisikika wakiimba "tuondokeni" kwa pamoja na kumtaka Rais wa Palestina, Mahmoud Abbas, ajiuzulu.

Taarifa zilisema mvutano huo uliongezeka wakati gari ndogo za Mamlaka ya Palestina zilipoingia ndani ya jiji, kwamba polisi walifyatua mabomu ya machozi na kurushiana risasi na waandamanaji.

"Walianza kufyatua risasi na watu wote wakaanza kukimbia. Watu walikuwa wakijitokeza tu kuunga mkono Gaza, lakini mamlaka ya Palestina haina uwezo wa kuwalinda raia wake dhidi ya ukandamizaji huu," alisema msichana mdogo ambaye ilidaiwa kuwa alipigwa risasi na kufariki kwa majeraha jioni ya juzi.

Sumaya Abdelrahman, mwanafunzi wa Kipalestina huko Beirut, anatoa wito kwa jumuiya ya kimataifa: "Ufaransa, Marekani, Uingereza wako wapi, lakini wanatazama wapi? Waisrael wanashambulia hospitali, haiwezekani! Kuna wagonjwa, watu waliojeruhiwa waliokuwa wakipewa huduma katika hospitali hiyo."

**DW, VOA, RFI**

# Uingereza yatoa hadhari kwa raia wake Uganda

**LONDON, Uingereza**

SERIKALI ya Uingereza imetoa tahadhari kwa raia wake wajiepushe kuitembelea mbuga mashuhuri ya wanyama nchini Uganda ambako watalii wawili, akiwamo raia mmoja wa Uingereza, anadaiwa kuuawa.

Maofisa wa polisi na wa mbuga ya wanyama walisema watu hao watatu walishambuliwa juzi na watu waliokuwa na bunduki wakati wakifanya safari katika mbuga ya kitaifa ya Malkia Elizabeth kusini magharibi mwa Uganda na gari yao kutiwa moto.

Shirika la Huduma za Wanyamapori la Uganda liliwatambua wahanga wengine wawili kama mtalii wa Afrika Kusini na mwongozaji safari wa Uganda.

Aidha, ilielezwa kuwa polisi wamelinyooshea kidole cha lawama kundi la Allied Democratic Forces (ADF) kwa shambulizi hilo.

Msemaji wa Polisi, Fred Enanga, alisema vikosi vyao vya pamoja vilichukua hatua baada ya kupokea taarifa na wanawatafuta washukiwa waasi wa kundi la ADF.

**DW**

# SERIKALI YAAHIDI KUWANOA WANAMICHEZO WANAWAKE

**Na Saada Akida**

KUELEKEA katika Tamasha la Michezo la Wanawake nchini, serikali imesema mwaka huu imewekeza nguvu zake zaidi katika kuandaa semina na mafunzo mbalimbali kwa wachezaji wa kike ili kuongeza ufahamu katika sekta hiyo, imeelezwa.

Tamasha hilo maarufu kwa jina la Tanzanite litafanyika Jumamosi na Jumapili kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kwa kushirikisha michezo mbalimbali.

Hata hivyo, tamasha hilo litatanguliwa na kongamano maalumu litakalofanyika kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere jijini.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo Taifa (BMT), Neema Msitha, alisema washiriki wa kongamano watapata elimu itakayowajengea uwezo katika masuala ya uongozi na namna ya kutangaza michezo yao pamoja na namna ya kupata wadhamini.

Msitha alisema kuna baadhi ya wachezaji wako katika michezo lakini wanatakiwa kujishughulisha na mambo ya kijamii ikiwamo biashara kwa ajili ya kujiongezea kipato. "Katika kongamano hilo kutokuwa na elimu kwa wanawake waliopo katika michezo hasa watoto wa kike kuwaeleza mbali na mpira au ngumi wanatakiwa kufanya kitu kingine katika jamii.

Wanawake wamekuwa wakiiletea heshima taifa letu kipindi wanapokwenda katika mashindano ya kimataifa, tumeshuhudia medali na makombe katika michezo mbalimbali ikiwamo gofu, ngumi na riadha, juhudi hizo pia tujikite katika kuwapa elimu mbali na kufanya michezo," alisema Msitha.

Aliongeza Tamasha la Tanzanite litakuwa na burudani kutoka kwa wasanii wa muziki wa bongo fleva wanawake pamoja na utoaji wa tuzo kwa wadau wa michezo ambao wametoa mchango.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, akizungumza namna jeshi hilo pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vilivyojipanga kuelekea mechi ya African Football League kati ya Simba dhidi ya Al Ahly kutoka Misri itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Kundemba yaipania Chipukizi FC

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kundemba imesema imejipanga kuhakikisha inaibuka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Chipukizi itakayochezwa leo kuanzia saa 10:15 kwenye Uwanja wa Mau A.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ali Vuai alisema wamefanya maandalizi mazuri kuelekea mechi hiyo kwa sababu malengo yao ni kuondoka na alama tatu wakiwa kwenye uwanja wa nyumbani.

Vuai alisema anajua mechi hiyo haitakuwa nyepesi kwa sababu anawafahamu vyema ubora wa Chipukizi FC lakini kikosi chake kimejipanga kupata ushindi katika mchezo huo.

Alisema sasa hivi timu yao imefanya maboresho katika safu ya ushambuliaji na ulinzi ili kuhakikisha wachezaji wake wanatimiza majukumu yao kama benchi la ufundi linavyowaelekeza.

"Hatukufanya vizuri kama michezo miwili iliyopita, hivyo lazima mchezo huu tuhakikishe tunapata alama tatu za kutuweka vizuri katika msimamo wa ligi, kimwonekano mchezo hautakuwa rahisi kwa sababu wenzetu nao wanataka alama tatu wakiwa ugenini," Vuai alisema.

Aliongeza kwa kuwataka mashabiki wa timu hiyo kuendelea kuiunga mkono timu yao kila inaposhuka dimbani.

Kundemba yenye pointi saba inashuka uwanjani ikiwa katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar wakati wapinzani wao Chipukizi yenye pointi 10 wako katika nafasi ya sita.

## Kocha Azam FC awajibu mashabiki

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi chake kikiendelea na maandalizi ya kuikabili Yanga, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema bado yupo sana katika timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Dabo ametoa kauli hiyo kutokana na baadhi ya mashabiki kudai kocha huyo angetimuliwa mapema katika kikosi hicho.

Kocha huyo raia wa Senegal alisema yeye ni mzoefu katika kazi hiyo na kila siku alikuwa anaamini atafikia malengo yake.

"Sikuwa na wasiwasi, nilijua Oktoba 14, Nyerere Day nitakuwa hapa, na waliposema vile niliwasikia, nilikuwa nacheka tu. Unajua hata wamiliki ilipofika Oktoba 14 walinitumia ujumbe kunikumbusha baadhi ya mashabiki walisema sitafika siku hii," alisema kocha huyo ambaye kwa sasa kikosi chake kinashika nafasi ya pili katika msimamo Ligi Kuu Tanzania Bara.

Azam FC itavaana na mabingwa watetezi, Yanga katika mechi ya mzunguko wa sita itakayochezwa Oktoba 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

## Twiga Stars yaota fainali ya WAFCON

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Esther Chabruma, amesema kikosi hicho kinaendelea kujifua kwa sababu kinahitaji kufanya vizuri katika mechi za mashindano yote zinazowakabili.

Twiga Stars inatarajia kuwakaribisha Botswana katika mechi ya kusaka tiketi ya kucheza Michezo ya Olimpiki itakayochezwa Oktoba 26, mwaka huu na kurudiana baada ya siku tano na itaivaa Togo kwenye mechi za kutafuta nafasi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON 2024).

Chabruma alisema kila mechi ni muhimu na kikosi chao kimekuwa katika mazoezi kwa muda mrefu kwa sababu wanahitaji kufikia malengo.

"Mechi zote ni ngumu, tunafanya mazoezi maalumu ya kuhakikisha tunapata ushindi katika kila mechi na hatimaye kusonga mbele, tunahitaji kuendelea kuipa heshima bendera ya Tanzania," alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa Twiga Stars.

Twiga Stars ilisonga mbele katika michuano ya Afrika baada ya kuwaondoa wenyeji Ivory Coast wakati Kenya iliwatupa nje Cameroon na Burundi ikawafunga Ethiopia.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS ANUKIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inatayarisha ofa ya kumnunua kiungo wa kati wa Manchester City na Timu ya Taifa ya England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 27. **(Mail)**

### PALHINHA ATAJWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich pia imezungumza na Manchester City kuhusu hali ya Kalvin Phillips, lakini kiungo wa Fulham na Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 28, anabakia kuwa mlengwa mkuu wa klabu hiyo ya Ujerumani. **(90 min)**

### BARCA, DE JONG KUTETA

MKURUGENZI wa Michezo wa Barcelona, Deco amewasiliana na mawakala wa Frenkie de Jong kujadili mpango wa kurefusha mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, lakini kiungo huyo wa kimataifa wa Uholanzi hana haraka ya kuanza mazungumzo. **(Sport)**

### BARCA MAMBO MAGUMU

DECO amesema itakuwa vigumu kwa Barcelona kuongeza wachezaji wapya kwenye kikosi chao wakati wa usajili wa Januari kwa sababu ya hali ya kifedha ya klabu hiyo. **(Mundo Deportivo)**

### LIVERPOOL YAMTAKA MUSIALA

LIVERPOOL ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England, zinazomsaka mshambuliaji wa Ujerumani, Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 20 ambaye mkataba wake na Bayern Munich utaendelea hadi mwaka 2026. **(Sport Bild)**

### INACIO ANUKIA EPL

LIVERPOOL ilituma maskauti kumtazama mlinzi wa Ureno na Sporting, Goncalo Inacio mwenye umri wa miaka 22 wakati wa mechi ya nchi yake dhidi ya Bosnia-Herzegovina. **(90 min)**

### OUEDRAOGO AINGIA SOKONI

KIKOSI cha Kocha, Jurgen Klopp pia ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England zinazomfuatilia kwa karibu kiungo wa Schalke, Assan Ouedraogo mwenye umri wa miaka 17. **(Sky Sports Germany)**

### SIR JIM SAFI UNITED

UNUNUZI wa Sir Jim Ratcliffe wa hisa asilimia 25 ya Manchester United hautarajiwi kupigiwa kura na bodi yao siku ya Alhamisi huku maelezo ya mwisho ya mkataba huo yakitatuliwa. **(Telegraph)**

### LINDELOF AANZA KUJIULIZA

BEKI wa Manchester United na Sweden, Victor Lindelof mwenye umri wa miaka 29, anatarajia klabu hiyo itazingatia kipengele cha kuongeza mwaka mmoja katika mkataba wake ikiwa imesalia miezi 12 katika mkataba wake wa sasa. **(90 min)**

### EVANS ALIHOFIA AFYA YAKE

MLINZI wa Manchester United, Jonny Evans mwenye umri wa miaka 35 amesema alihofia angelazimika kustaafu soka kwa sababu ya majeraha msimu uliopita kabla ya kurejea Manchester msimu wa joto. **(90 min)**

### MITCHELL ANUKIA UNITED

ALIYEKUWA mkuu wa kitengo cha kuajiri wa Tottenham Hotspur, Paul Mitchell anapendekezwa kuwa mkurugenzi mpya wa soka katika klabu ya Manchester United, jambo ambalo linaweka kazi ya mkurugenzi wa sasa wa kandanda, John Murtough hatarini. **(The I)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DI MARIA ATANGAZA KUSTAAFU KIMATAIFA

●●●Ni baada ya kuichezea Argentina katika Copa America 2024...

**BUENOS AIRES, Argentina**

WINGA wa Argentina, Ángel Di María amesema michuano ya Copa America 2024 itakuwa mashindano yake ya mwisho akiwa na Albiceleste hao, akihitimisha mbio za miaka 16 ya kuitumikia timu ya taifa.

"Nitaondoka kwenye Timu ya Taifa ya Argentina baada ya Copa America. Imekwisha kwangu, itakuwa michuano ya mwisho," alisema mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiiambia redio ya Argentina Urbana Play 104.3.

Di Maria, ambaye hayumo katika kikosi cha Argentina kwa ajili ya mechi za kufuzu za CONMEBOL wiki hii kutokana na jeraha, alisema moja ya sababu za kurejea Benfica, timu ambayo ilimtambulisha Ulaya mwaka 2007 akitokea Juventus ilikuwa kumsaidia kufikia Copa America mwakani katika hali nzuri.

"Nilikuja Benfica kudumisha chaguzi zangu za kuendelea katika timu ya taifa," aliongeza Di Maria.

"Nilijua ni lazima nicheze katika timu nzuri ili niwe katika kiwango kizuri. Nataka kucheza Copa America ijayo na ninafanya kila niwezalo kuwa bora katika klabu yangu na kila ninapoichezea Argentina."

Michuano ya Copa America 2024 itafanyika kati ya Juni 20 na Julai 14, mwakani nchini Marekani.

Di Maria alikuwa shujaa kwa nchi yake baada ya kufunga mabao katika fainali mbili ambazo Argentina ilishinda mataji katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Alifunga bao pekee dhidi ya Brazil katika fainali ya Copa America mwaka 2021 na la kwanza kwa timu yake katika ushindi dhidi ya Ufaransa kwenye fainali ya Kombe la Dunia 2022.

"Nilisema mara nyingi kwa familia yangu, Copa America ilibadilisha maisha yetu milele," alisema Di María.

"Kwa sababu ilikuwa mara zote kufika huko kwenye fainali na kushindwa, hadi siku niliporudi nyumbani na waliniambia 'wakati huu umeshinda'.

"Baada ya kuwa bingwa wa dunia, watu wanakutambua kila mahali. Ninapeleka binti zangu shuleni nchini Ureno na kuna watoto ambao wana umri wa miaka mitano au sita na wananiambia: 'Wewe ni bingwa wa dunia.' Hilo ndilo jambo pekee wanalojua kunihusu."

Di María, ambaye aliwahi kuzichezea Paris Saint-Germain, Manchester United na Real Madrid katika maisha yake ya soka barani Ulaya, ameifungia Argentina mabao 29.

Mbali na mataji ya Kombe la Dunia na Copa America, alishinda medali ya dhahabu huko Beijing 2008 akiwa na Argentina na Kombe la Dunia la FIFA U-20 mnamo 2007.

# BELLINGHAM ATAKA KUZEEKEA MADRID

**MADRID, Hispania**

JUDE Bellingham amesema anataka kubakia Real Madrid kwa "miaka 10 hadi 15" ijayo baada ya kudai timu hiyo ya Ligi Kuu Hispania (LaLiga), imesaidia kupeleka mchezo wake katika kiwango kipya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 alicheza nafasi kubwa katika ushindi wa mabao 3-1 wa England dhidi ya Italia kwenye Uwanja wa Wembley hapo juzi akiwasaidia Simba Watatu hao kupata nafuu baada ya bao la kwanza la Gianluca Scamacca dakika ya 15 na kufanikiwa kupata ushindi ambao uliwafanya wafuzu Euro 2024.

Kane aliongeza bao la tatu la dakika za mwisho na kuipa England ushindi wa kwanza dhidi ya Italia katika ardhi ya nyumbani tangu 1977, na kulipiza kisasi kwa kushindwa kwao fainali ya Euro 2020 na wapinzani wao hao miaka miwili iliyopita.

Bellingham sasa ana mabao 11 na asisti sita katika mechi 13 za klabu na nchi msimu huu kufuatia uhamisho wake wa majira ya joto kutoka Borussia Dortmund kwa ada ya awali ya euro milioni 103.

Na aliiambia Channel 4: "Ninaimarika kidogo kila ninapocheza. Ulikuwa usiku mzuri sana kwetu, sote tunakumbuka kilichotokea miaka michache iliyopita walipocheza hapa. Siku zote unalenga maendeleo. Sisi kuelekea katika mwelekeo sahihi na ushindi muhimu sana kwetu.

"Napenda soka kwa sasa. Uongozi wangu katika klabu na nchi unanipa uhuru wa kuucheza jinsi ninavyouona.

"Tangu miezi michache iliyopita nimekuwa nikifanyia kazi muda wangu wa kuingia kwenye boksi na ninapowasili nawasili na njaa kali.

"Pamoja na uhamisho mkubwa ukweli ni kwamba ni lazima nifanye, iwe ni bao au pasi ya mabao au ushindi wa mechi.

"Hii ndiyo klabu ninayotaka kuwa nayo kwa miaka 10 hadi 5 ijayo ya maisha yangu."



## Sane kurejea England Januari

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Liverpool imeripotiwa imeweka kipaumbele kumnasa winga wa Bayern Munich, Leroy Sane, awe mirithi wa Mohamed Salah ambaye anatarajiwa kutimkia Saudi Arabia.

Kwa mujibu wa gazeti la The Mirror, Liverpool inajipanga kuvunja rekodi ya uhamisho katika historia ya klabu hiyo katika mchakato wa kumnasa Sane.

Rekodi ya uhamisho katika klabu hiyo hivi sasa inashikiliwa na Darwin Nunez, aliyetua kwa pauni milioni 64.2 na nyongeza ya pauni milioni 21.4, akitokea klabu ya Benfica mwaka 2022.

Ikiwa mambo yatakwenda kama yalivyopangwa, miamba hiyo italipa zaidi ya fedha ilizomnasa Nunez, ili kumsajili Sane.

Hata hivyo, Bayern inaweza kuweka ngumu kumpoteza Sane ambaye amefunga mabao sita katika mechi saba za Ligi Kuu Ujerumani msimu huu 2023/24.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp ameripotiwa anavutiwa na Sane na anataka kumrudisha katika michuano ya Ligi Kuu England (EPL).

Wakati alipokuwa akikipiga Manchester City, Sane alishinda mataji mawili ya Ligi Kuu England, Kombe na FA na mataji matatu ya Kombe la Ligi.

Salah ameanza msimu huu kwa kiwango kizuri akifunga mabao matano na kutoa pasi nne za mabao katika mechi nane za Ligi Kuu England.

Inatarajiwa nyota huyo kutoka nchini Misri mwenye umri wa miaka 31, anaweza kutimka katika kikosi hicho Januari mwakani na kuelekea Ligi Kuu Saudi Arabia.

Nyota huyo alikuwa akihusishwa kwa kiasi kikubwa kwenda Saudi Arabia katika majira ya kiangazi mwaka huu, kufuatia klabu ya Al Ittihad kutuma ofa ya Pauni Milioni 150, lakini Liverpool ilipiga chini.

Katika kikosi cha Liverpool, Salah amecheza michezo 315 na kufunga mabao 192.

## Kroos akaribia kutua City

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City inalenga kumsajili mwamba wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Toni Kroos na ipo tayari kumlipa pauni milioni 13 kwa mwaka ili tu asaini kukipiga Etihad.

Timu hiyo inayonolewa na Pep Guardiola ilibeba taji lake la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, wakati ilipoweka rekodi ya kunyakua mataji matatu makubwa ndani ya msimu mmoja.


Lakini, sasa anahusishwa na mpango wa kumchukua mchezaji mwenye uzoefu zaidi na dili hilo litafanyika mwishoni mwa msimu huu.

Mjerumani huyo akitua tu Etihad basi mshahara wake atalipwa karibu mara mbili ya kile kiwango anachopokea huko Bernabeu.

Kroos (33), alijiunga na Madrid akitokea Bayern Munich mwaka 2014 na mahali hapo amebeba karibu kila taji aliloshindania.

Amenyakua Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tano, likiwamo moja alilobeba Bayern, La Liga mara tatu na Klabu Bingwa Dunia mara nne. Mkataba wake wa sasa utafika tamati Juni 2024.

Huko Bernabeu, Kroos kwa sasa analipwa pauni milioni 6.8 kwa mwaka, lakini City itamlipa pauni milioni 13 na itampa dili la miaka miwili.



# GAMONDI AWATEGA SKUDU, KONKON 'AKIWAOTA' AZAM

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikijiandaa na mchezo dhidi ya Azam FC, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi amewataka nyota wake wawili, Hafiz Konkoni na Mahlatsi Makudubela 'Skudu' kuonyesha kiwango kizuri kwa lengo la kubakia katika kikosi cha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara.

Gamondi amewataka wachezaji hao kuimarika na endapo hawatabadilika, atalazimika kufanya uamuzi 'mgumu' wakati wa dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa ifikapo Desemba.

Kocha huyo amesema tangu wachezaji hao wajiunge na Yanga, hawajaweza kutimiza matarajio ya klabu kwa kuweka wazi Skudu ameshindwa kuitendea haki jezi namba sita aliyokabidhiwa huku Konkoni naye ameshindwa kuvaa viatu vya mshambuliaji aliyeondoka, Fiston Mayele.

Taarifa za uhakika zilizoifikia Nipashe jana, kuwa kocha Gamondi hatokuwa tayari kuendelea nao kama hawatoongeza viwango vyao kabla ya kufikia kipindi cha dirisha dogo.

Chanzo cha kuaminika kutoka ndani ya Yanga kimeliambia Nipashe tayari Gamondi ameshawasilisha majina ya wachezaji ambao anataka waachwe wakati wa dirisha dogo.

Taarifa zaidi zinasoma kocha huyo amewaambia mabosi wa Yanga kusaka mshambuliaji mwingine ambaye ataweza kuisaidia timu katika mechi za hatua ya makundi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa sababu kwa sasa hana mchezaji mwenye makali ya kupenya ngome za wapinzani.

"Mwalimu amewasilisha majina ya nyota ambao anataka wapunguzwe na alichofanya ni kumtaka kila mmoja kuongeza kiwango chake wakati huu kabla ya dirisha dogo na kama hali itaendelea hivyo basi hatokuwa tayari kubaki nao.

Unajua presha ya ndani imekuwa kubwa ndiyo maana benchi la ufundi limefanya tathmini ya kina, kuna uwezekano mkubwa wa kufanya marekebisho ili kufikia malengo na litakuwa jambo gumu kuwa na timu ambayo haina mshambuliaji halisi," kilisema chanzo chetu.

Nipashe lilipowasiliana na kocha huyo alikiri anataka kuona kila mchezaji anajituma ili kufikia malengo ya kuisaidia timu na hatokuwa tayari kuona wachezaji wenye viwango vidogo wanabakia klabuni hapo.

Katika hatua ya makundi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Yanga iko pamoja na Al Ahly ya Misri, Medeama (Ghana) na CR Belozdad ya Algeria.



Mashabiki wa Simba wa Temeke Stereo, Dar es Salaam wakicheza ngoma kwa lengo la kuhamasisha kuelekea mechi ya ufunguzi ya michuano ya African Football League (AFL), dhidi ya Al Ahly kutoka Misri itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: SIMBA SC**

# Tamasha la Muziki Afrika Acces laiva

**Na Faustine Feliciane**

TAMASHA la muziki linalofanyika pamoja na kongamano la wasanii pamoja na wafanyabiashara wa sekta ya muziki litafanyika tena kuanzia Novemba 9 hadi 11, mwaka huu hapa nchini.

Tamasha hilo linaloandaliwa na Taasisi ya Music in Africa Foundation (MIAF) linafanyika kwa mara ya pili na litashirikisha zaidi ya wasanii 40 kutoka ndani na nje ya nchi huku likitarajiwa kutoa fursa kwa wasanii wa ndani kujifunza na kubadilishana ujuzi kutoka kwa wasanii wakubwa.

Pia wasanii wa Kitanzania watakutana na watayarishaji wa kimataifa huku pia wakipata nafasi nyingine ya kunadi kazi zao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa MIAF, Eddie Hatitye alisema tamasha hilo pia litatoa fursa kwa wageni kutembelea maeneo mbalimbali ya vivutio hapa nchini.

Alisema miongoni mwa watu mashuhuri watakaoshiriki kwenye kongamano hilo ni pamoja na msanii na mjasiriamali kutoka Afrika Kusini, Sho Madjozi atakayefanya mahojiano na Kituo cha Sauti ya Amerika.

Aliwataja watu wengine mashuhuri watakaoshiriki ni pamoja na mwanzilishi wa Symphony OS, Chuka Chase kutoka Marekani, mwanzilishi wa Roxanne Sonia, Boton-Gboh (Ufaransa), Ofisa Maendeleo wa Kimataifa wa SACEM Afrika, Akotchayé Okio (Ufaransa) na Mkurugenzi Mkuu wa Sony Music Publishing, Rowlin Naicker (Afrika Kusini).

Wanamuziki wengine watakaoshiriki ni Marioo (Tanzania), Siti Muharamna na bendi ya 'The Unguja All Stars' (Tanzania), Ngwaka Son Systéme (DRC), Nour Harkati (Tunisia), Zolani Mahola & The Feminine Force (Afrika Kusini), Alostmen (Ghana), Feli Nandi (Zimbabwe), Leo Mkanyia (Tanzania), Kasiva Mutua (Kenya), Madalitso Band (Malawi) na Damian Soul (Tanzania), Dulla Makabila, Damian Soul wa Tanzania.

Naye Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), Dk. Kedmon Mapana amewataka wasanii wa hapa nchini kuchangamkia fursa hiyo kwa kujiandikisha kushiriki kwenye kongamano na tamasha hilo.

"Muziki ni biashara, wasanii wa hapa nchini hii ni fursa nyingine kwao, wajiandikishe mapema ili kukutana na watu wakubwa katika muziki na kupata ujuzi," alisema Mapana.

Alisema kufanyika kwa mara ya pili kwa tamasha hilo kumetokana na mazingira mazuri yaliyowekwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuendeleza sanaa na michezo nchini.

## Rais Samia anogesha mechi ya Simba AFL

INATOKA UK. 24

ezo huo ili kutoweka dosari katika mechi hiyo ya ufunguzi wakiangalia Al Ahly ni timu kubwa na wanawaheshimu lakini wako tayari kuonyesha soka safi dhidi yao.

"Niwaombee waje kwa wingi kuwasapoti kwa maana wanunue tiketi, nimeangalia leo (jana), tumefika katika hatua nzuri ya ununuzi wa tiketi, maandalizi yaliyofanyika ndani ya uwanja hayajawahi kutokea, maandalizi haya ya ufunguzi yanatakiwa kuwa kama Kombe la Dunia.

Al Ahly atakufa nyingi siku hiyo, bado uwezo wetu upo juu ndiyo maana FIFA wameona Tanzania ndiyo sehemu sahihi kufanya ufunguzi," aliongeza bosi huyo.

Mabosi wengine wa soka wanaotarajia kuhudhuria ufunguzi huo ni pamoja na Rais wa CAF, Patrice Motsepe, Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger na Fatma Samoura ambaye ni Katibu Mkuu wa FIFA.

Kutokana na ugeni huo, Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa sasa umekuwa na ulinzi mkali.

## Yanga yaihofia Azam FC

INATOKA UK. 24

mara kwa mara hufungwa na Yanga.

"Haitakuwa mechi nyepesi kwa sababu Azam FC watataka kujiuliza kwa nini huwa tunawafunga mara kwa mara, hasa kwenye mechi iliyopita ya Ngao ya Jamii, lakini sisi kama wachezaji tunalifahamu hilo na tutakwenda kwa tahadhari, hata kocha analifahamu hilo ndiyo maana anatuandaa vizuri akitupa mbinu, mifano, ubora na udhaifu wa Azam na tumekuwa tukivifanyia kazi mazoezini," alisema Mauya.

Jonas Mkude, alisema itakuwa mechi nzuri sana kwa sababu itazikutanisha timu kubwa nchini Tanzania.

"Mchezo utakuwa mgumu lakini sisi tumejiandaa kufanya vizuri, katika mazingira ya ligi yetu Azam ni timu kubwa kama Yanga, hivyo litakuwa bonge moja la mechi, sisi kwa upande wetu tunajiandaa vizuri kwa pambano hilo," Mkude, kiungo wa timu hiyo aliongeza.

Katika mechi ya mwisho kukutana, Yanga ilishinda mabao 2-0, wafungaji wakiwa ni Stephane Aziz Ki na Clement Mzize.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 19, 2023

Nipashe




Di Maria atangaza kustaafu kimataifa UKURASA 21

# RAIS SAMIA ANOGESHA MECHI YA SIMBA AFL

## ●●●Kununua bao kwa Sh. mil. 10, Mo aahidi donge nono endapo...



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda (kulia), akiwa katika vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao umefanyiwa marekebisho kuelekea mechi ya African Football League kati ya Simba dhidi ya Al Ahly itakayochezwa kesho. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameahidi kutoa Sh. milioni 10 kwa kila goli litakalofungwa na wachezaji wa Simba katika mechi ya ufunguzi wa michuano ya African Football League (AFL) dhidi ya Al Ahly itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mbali na Rais Samia, Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohamed Dewji (Mo), naye amewaahidi wachezaji wa timu hiyo donge nono iwapo itaibuka na ushindi katika mchezo huo.

Akizungumza katika uhamasishaji kuelekea mechi hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, alisema Rais Samia ameahidi kutoa kiasi hicho cha fedha endapo Simba itapata ushindi.

Msigwa alisema ahadi hiyo itaendelea pia katika kila mechi ambayo Simba itashinda katika michuano hiyo kama itasonga mbele.

“Wakati nakuja huku nimeongea na mheshimiwa Rais, kaniambia nenda kawahamasishe Wanasimba na Watanzania wote, mechi hii ni ya Watanzania, lakini akaniambia japokuwa hakuwa amesema kabla, lakini katika michuano hii ya AFL, mheshimiwa Rais ameahidi kila mechi watakayoshinda, kila goli atatoa Sh. milioni 10. Kwa kishindo na ubora wa michuano hii ameamua kuongeza, “ alisema Msigwa.



> **“Wakati nakuja huku nimeongea na mheshimiwa Rais, kaniambia nenda kawahamasishe Wanasimba na Watanzania wote, mechi hii ni ya Watanzania, lakini akaniambia japokuwa hakuwa amesema kabla, lakini katika michuano hii ya AFL, mheshimiwa Rais ameahidi kila mechi watakayoshinda, kila goli atatoa Sh. milioni 10. Kwa kishindo na ubora wa michuano hii ameamua kuongeza, “ alisema Msigwa.**

Katibu Mkuu huyo aliongeza mechi hiyo itakuwa ya kihistoria, hivyo amewataka Watanzania kujitokeza kwa wingi ili kuionyesha dunia jinsi gani Watanzania wanapenda soka.

“Simba wametuheshimisha kucheza hii michuano, kupata sifa ya kucheza michuano hii kumeipa pia sifa Tanzania kuwa nchi ya kwanza kufungua michuano hii, ni jambo kubwa linaloiletea sifa nchi yetu, nimekuja hapa Mbagala tuhamashishane, ni mechi kubwa Watanzania tujitokeze, tuonyeshe Afrika, tuionyeshe dunia nzima Tanzania na wananchi wake wanaupenda mchezo wa mpira wa miguu,” alisema Msigwa.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah, ‘Try Again’, amesema Mo amewaahidi wachezaji wa timu hiyo kiasi kikubwa cha fedha endapo watashinda mechi hiyo ya kihistoria inayotarajiwa kukutanisha watu mbalimbali maarufu wa mpira duniani, akiwamo Rais wa Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), Gianni Infantino.

Salim amesema mchezo huo ni muhimu sana na tayari wameshazungumza na wachezaji na benchi la ufundi ambao wameahidi wako tayari kuonyesha kandanda safi.

Alisema wazo la FIFA kuanzisha michuano hiyo ni faraja kubwa kwa Watanzania, mara ya kwanza kufanyika Tanzania na wanahitaji kuonyesha ukubwa wao kwa kushinda mchezo huo.

“Mara ya kwanza yanafanyika nchini, ufunguzi tutapokea ugeni mwingi kutoka familia ya soka duniani, kama Simba tumefurahi kuwa sehemu ya ufunguzi wa mashindano hayo.

Maandalizi yanaendelea vizuri, wachezaji walioenda timu zao za taifa wamesharudi kujiunga na wenzao, morali imeongezeka, hamasa imeongezeka tukiangalia wako tayari kupambana,” alisema Try Again.

Aliongeza wanahitaji kushinda mch-

INAENDELEA UK. 23

# Yanga yaihofia Azam

**Na Adam Fungamwango**

ILI kujihakikishia ushindi, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema wataikabili Azam FC kwa tahadhari katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Gamondi amesema anafahamu Azam FC wataingia tofauti na watahitaji kulipiza kisasi kutokana na kuwafunga katika mechi ya Ngao ya Jamii.

Kocha huyo alisema anafahamu rekodi za hivi karibuni haziwabebi Azam, hivyo anaiona mechi ya Jumapili itakuwa ngumu na wapinzani wao hawataingia uwanjani kinyonge.

Alisema kwa sasa wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi hiyo lakini akifanyia kazi ubora na udhaifu wao.

“Nadhani hapa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara nimeona hakuna mechi rahisi, hasa timu zinapocheza na Yanga, na ukiangalia Azam ni timu nzuri, hata mchezo ule tulicheza Tanga ulikuwa mgumu sana, uliona kipindi cha pili katika mechi ile tulicheza vizuri sana lakini ulikuwa mchezo mgumu na wa kipekee,” alisema kocha huyo.

Aliweka wazi wataingia uwanjani kwa tahadhari na amewaelekeza wachezaji wake ni aina gani ya mfumo wanaotakiwa kucheza dhidi ya timu hiyo ili kupata ushindi.

Naye kiungo mkabaji wa timu hiyo, Zawadi Mauya, amekiri mechi hiyo haitakuwa nyepesi kama watu wanavyodhani kwa sababu wapinzani wao watataka kujiuliza ni kwa nini

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >